# UCHANGANUZI WA ATHARI ZA KIMOFOFONOLOJIA MIONGONI MWA WANAFUNZI WA KISOMALI WANAPOJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI

**AMOS KATIVA MANUNDU**

**Tasnifu iliyowasilishwa ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Pwani**

**Augosti, 2019**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mimi mwenyewe wala haijawahi kamwe kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa minaji ya kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote ile.

Amos Kativa Manundu

C50/IB/PU/3172/2014

Sahihi ____________________ Tarehe 8/09/2020

Tunathibitisha kuwa kazi iliyowasilishwa katika tasnifu hii ya shahada ya uzamili ilifanywa na mtahiniwa chini ya usimamizi wetu. Hakuna sehemu ya tasnifu hii ambayo itatolewa kwa namna yoyote ile bila ya kibali kutoka kwa mwandishi na Chuo Kikuu cha Pwani.

Wasimamizi:

Dkt. Nancy JumwaNgowa .

Chuo Kikuu Pwani –Kenya.

Sahihi____________________ Tarehe 08/09/2020

Prof. Rocha Chimerah.

Chuo Kikuu Pwani –Kenya.

Sahihi____________________ Tarehe 9.9.20

## TABARUKU

Naitabarukia kazi hii kwa mwanangu Mûuw'o, mke wangu Mukeli na mamangu Fidelis kwa imani waliyokuwa nayo katika uwezo wangu na kwa kunihimiza kutia bidii.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili na pia kuikamilisha kazi hii. Ningependa kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kwa njia moja au nyingine katika ufanisi wa utafiti huu. Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Nancy Ngowa na Prof. Rocha Chimerah ambao waliniongoza kutoka mwanzo hadi nilipoikamilisha kazi hii. Daima nawatakia kheri na baraka zake Mterehemezi.

Natoa shukrani kwa walimu wa shule za upili za County, NEP, Tetu, Umu Salama, BoysTown na Yathrib kwa kuniruhusu kutangamana na wanafunzi wao na kupata data iliyofanikisha utafiti huu. Bw. Mohamed Abdikarim, mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Sankuri nashukuru kwa kuniruhusu kwenda nyanjani kila mara.

Kwa mama mzazi umekuwa katika mstari wa mbele kunihimiza kulenga juu masomoni na pia kunifadhili kwa hali na mali kuhakikisha nimefaulu asante sana. Ninajua kunao wengi waliochangia ambao sijawataja, kwenu nyote nasema, ahsante.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kisomali wanapojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Utafiti huu ulifanywa katika shule za upili za umma katika kaunti–ndogo ya Garissa-Township, Garissa kaunti, nchini Kenya. Lugha ya Kisomali imefanyiwa utafiti katika vipengele mbalimbali katika maeneo tofautitofauti lakini hakuna utafiti ambao umewahi kufanywa katika maeneo ya Garissa. Basi utafiti huu ulilenga kuziba mwanya huu wa kielimu hasa katika kiwango cha kimofofonolojia katika lugha ya Kisomali, eneo la Garissa.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (N.U.M) ambayo iliasisiwa na Corder mwaka wa 1967, ambaye anasema kuwa kufanya kosa ni njia mojawapo ya kujifundisha lugha ya pili. Kwa hivyo, mwanafunzi anapofanya kosa, asiadhibiwe bali chanzo cha kosa kibainishwe.

Data iliyohusishwa ilitoka nyanjani na ilikuwa makosa ya kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili yanayofanywa na wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kisomali kutoka shule za upili za umma za kaunti-ndogo ya Garissa-Township. Data ya nyanjani ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya kuandika insha na kusimulia hadithi ambapo wanafunzi wa kidato cha tatu waliokuwa wameteuliwa waliandika insha na kusimulia hadithi. Wanafunzi hawa waliteuliwa kwa sababu walikisiwa kuwa wamepata umilisi wa lugha ya Kiswahili na hawakuwa katika pilka pilka za kujiandaa kwa mtihani wa kitaifa. Mtafiti alikusanya insha ili kuzisoma na kanda alizokuwa amerekodi ili kuzisikiliza na kutambua makosa ya kimofofonolojia yaliyofanywa na wanafunzi. Hii ndio ilikuwa data ya utafiti.

Data ilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa maelezo. Vifaa tulivyotumiwa ni insha na hadithi.

Katika sura ya kwanza, tulielezea usuli wa mada, umuhimu wa utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na upeo wa mipaka. Sura ya pili tulielezea misingi ya kinadharia iliyotuongoza katika ukusanyaji na uchambuzi wa data, maandiko mbalimbali tuliopitia yanayohusiana na mada hii, dhana ya fonolojia ya Kiswahili, fonolojia ya Kisomali, fonimu, mofimu na mofofonolojia. Sura ya tatu ilishughulikia utaratibu wa utafiti, jumuia na uteuzi wa sampuli, eneo la utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na maadili ya utafiti.
Sura ya nne ilishughulikia uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia pamoja na kueleza sababu zinazowafanya wanafunzi kufanya makosa haya. Makosa yaliorodheshwa na kupangwa katika makundi tofauti na sehemu ambamo yanapatikana. Makosa haya yaliainishwa baada ya insha za watafitiwa kusahihishwa ili kubaini makosa ya kimofofonolojia yalivyojitokeza kutokana na data tuliyokusanya. Katika sura ya tano, mtafiti ameeleza hitimisho na mapendekezo.

Utafiti huu ni hazina kubwa kwa elimu ya Isimu ya lugha za Kiafrika. Utafiti katika lugha ya Kisomali umeiweka lugha hiyo katika ramani ya ulimwengu na hali hii inaendeleza lugha mahsusi kiusomi.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| N.U.M | Nadharia ya Uchanganuzi Makosa |
| L1 | Lugha ya kwanza |
| L2 | Lugha ya pili |

## MAELEZO YA ISTILAHI

Istilahi zifuatazo zilitumika katika utafiti huu na zilifafanuliwa kama ifuatavyo:

**Lugha ya kwanza** : Ni lugha ambayo mtoto hujifunza kwa mara ya kwanza. Pia hurejelewa kama lugha asilia au lugha ya mama.

**Lugha ya pili** : Ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha yake ya kwanza.

**Makosa** : Kulingana na kazi hii neno hili limetumika kwa maana ya kanuni ambayo imekwenda kinyume na kanuni zilizowekwa. Kanuni isiyo sahihi.

**Uchanganuzi Makosa** : Ni mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi. Mbinu hii huchunguza aina ya makosa na visababishi vya makosa hayo. Ni njia ya kupambanua, kuainisha na kufafanua makosa yanayofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili.

**Wasemaji** : Kwa kazi hii imetumika kwa maana ya wazungumzaji wa lugha ya kwanza.

**Kujifunza lugha** :Ni kupata ufahamu wa lugha katika mazingira rasmi kwa kufundishwa kufuata utaratibu wa silabasi na kwa kupewa mazoezi.

## YALIYOMO

UNGAMO .......... ii

TABARUKU .......... iii

SHUKRANI .......... iv

IKISIRI .......... v

ORODHA YA VIFUPISHO .......... vii

MAELEZO YA ISTILAHI .......... viii

ORODHA YA MICHORO .......... xiv

ORODHA YA MAJEDWALI .......... xv

SURA YA KWANZA .......... 1

UTANGULIZI .......... 1

1.1 Kitangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Mada .......... 1

1.3 Swala la Utafiti .......... 6

1.4 Madhumuni ya Utafiti .......... 7

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 7

1.6 Upeo na Mipaka .......... 7

1.7 Umuhimu wa Utafiti .......... 8

SURA YA PILI .......... 10

MAPITIO YA MAANDIKO .......... 10

2.1 Kitangulizi .......... 10

2.2 Misingi ya Nadharia ........................................................................................ 10

2.3 Mapitio ya kazi Mbalimbali ................................................................................ 12

2.3.1 Makosa yanayojitokeza mwanafunzi anapojifunza lugha ya Kiswahili ..................... 12

2.4 Dhana ya Fonolojia ............................................................................................ 25

2.5 Dhana ya Fonimu ............................................................................................... 26

2.5 Irabu za Kiswahili ............................................................................................... 27

2.6 Konsonanti za Kiswahili ...................................................................................... 29

2.7 Dhana ya Mofimu ............................................................................................... 34

2.8 Fonolojia ya Kisomali ......................................................................................... 35

2.9 Fonimu za Irabu za Kisomali ................................................................................ 37

2.10 Fonimu za konsonanti za Kisomali ....................................................................... 38

2.11 Dhana ya Mofolojia ............................................................................................ 39

2.12 Dhana ya Mofofonolojia ...................................................................................... 40

SURA YA TATU ...................................................................................................... 42

MBINU ZA UTAFITI ................................................................................................. 42

3.1 Kitangulizi .......................................................................................................... 42

3.3 Utaratibu wa Utafiti .............................................................................................. 43

3.4 Jumuiya na Uteuzi wa Sampuli ............................................................................. 43

3.5 Vifaa vya Kukusanyia Data ................................................................................... 44

3.5.1 Insha ................................................................................................................ 44

3.5.2 Hadithi ............................................................................................................. 45

3.6 Ukusanyaji wa Data ........................................ 45
3.7 Uchanganuzi wa Data ........................................ 45
3.8 Maadili ya Utafiti ........................................ 46
SURA YA NNE ........................................ 47
UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO ........................................ 47
4.1 Kitangulizi ........................................ 47
4.2 Kukusanya Sampuli ya wanaojifunza Lugha ........................................ 48
4.3 Kutambua Makosa ........................................ 49
4.4 Kueleza Makosa kwa kuyaweka katika Makundi ........................................ 49
4.5 Kuhesabu Makosa. ........................................ 49
4.6 Mageuzi ya vokali ........................................ 50
4.6.1 Udondoshaji wa vokali ........................................ 50
4.6.1.1 Udondoshaji wa /i/ ........................................ 51
4.6.1.2 Udondoshaji wa /a/. ........................................ 51
4.6.1.3 Udondoshaji wa irabu /ɛ/. ........................................ 52
4.6.1.4 Udondoshaji wa irabu /u/ ........................................ 53
4.6.2 Ubadala wa Vokali ........................................ 53
4.6.2.1 Ubadala wa irabu /i/ > /ɛ/ ........................................ 54
4.6.2.2 Ubadala wa irabu /a/ >/ɔ/. ........................................ 54
4.6.2.3 Ubadala wa irabu /u/ > /ɔ/ ........................................ 55
4.6.2.4 Ubadala wa /ɛ/ > /i/. ........................................ 56

4.6.2.5 Ubadala wa vokali /ɛ/ > /a/ ........ 56

4.6.2.7 Ubadala wa /ɔ/ > /ɛ/. ........ 57

4.7 Mageuzi ya Konsonanti ........ 59

4.7.1 Ubadala wa konsonanti ........ 59

4.7.1.1 Ubadala wa /ʃ/> /č/........ 59

4.7.1.2 Ubadala wa konsonanti /b/ > /p/ ........ 60

4.7.1.3 Ubadala wa /p/ > /b/........ 60

4.7.1.4 Ubadala wa /č/ > /ʃ/........ 62

4.7.1.5 Ubadala wa /ð/ > /Ɵ/........ 62

4.7.1.6 Ubadala wa /s/ > /z/. ........ 63

4.7.1.7 Ubadala wa /z/ > /s/. ........ 64

4.7.1.9 Ubadala wa /ɲ/ > /j/........ 64

4.7.1.10 Ubadala wa /ʃ/ > /s/........ 65

4.7.1.11 Ubadala wa /f/ > /b/ ........ 66

4.7.1.12 Ubadala wa /v/ > /f/ ........ 66

4.7.1.13 Ubadala wa /g/ > /k/........ 67

4.7.2.1 Uchopekaji wa konsonanti........ 67

4.7.2.2Uchopekaji wa /j/........ 68

4.7.2.3 Uchopekaji wa /w/ ........ 68

4.7.2.4 Uchopekaji wa /n/ ........ 69

4.7.2.5 Uchopekaji wa /h/ ........ 69

4.7.3.1 Udhoofikaji kwa konsonanti....70
4.7.3.2Kudhoofika kwa konsonanti /j/ hadi irabu /i/....70
4.7.3.3 Kudhoofika kwa /w/ hadi irabu /u/....71
4.8 Maelezo ya Matokeo ya Data....71
4.8.1 Ubadilishaji....72
4.8. Udondoshaji....75
4.9 Uchopekaji....76
4.11 Kihitimisho....77
SURA YA TANO....79
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....79
5.1 Kitangulizi....79
5.2 Hitimisho....79
5.3 Mapendekezo....80
MAREJELEO....82

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Irabu za Kiswahili ........ 28

Mchoro 2: Jinsi /a/ inavyosawiriwa na kuwa irabu tofauti ........ 58

Mchoro 3: Jinsi /ɛ/ inavyosawiriwa na kuwa vokali tofauti ........ 58

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1 : Konsonanti za Kiswahili .......... 34

Jedwali 2 : Fonimu za konsonanti za Lugha ya Kisomali .......... 37

Jedwali 3 : Fonimu za konsonanti za lugha ya Kisomali .......... 38

Jedwali 4: Udondoshaji wa /i/ .......... 51

Jedwali 5 : Udondoshaji wa /a/ .......... 52

Jedwali 6: Udondoshaji wa irabu /ɛ/. .......... 52

Jedwali 7: Udondoshaji wa irabu /u/. .......... 53

Jedwali 8: Ubadala wa irabu /i/ > /ɛ/ .......... 54

Jedwali 9: Ubadala wa irabu /a/ > /ɔ/ .......... 55

Jedwali 10: Ubadala wa irabu /u/ > /ɔ/. .......... 55

Jedwali 11: Ubadala wa /ɛ/ > /i/ .......... 56

Jedwali 12: Ubadala wa vokali /ɛ/ > /a/ .......... 57

Jedwali 13: Ubadala wa /ɔ/ > /ɛ/ .......... 57

Jedwali 14: Ubadala wa /ʃ/ > /čh/ .......... 59

Jedwali 15: Ubadala wa konsonanti /b/ > /p/ .......... 60

Jedwali 16: Ubadala wa /p/ > /b/ .......... 61

Jedwali 17: Ubadala wa /čh/ > /ʃ/ .......... 62

Jedwali 18: Ubadala wa /đ/ > /Ɵ/. .......... 63

Jedwali 19: Ubadala wa /s/ > /z/ .......... 63

Jedwali 20: Ubadala wa /z/ > /s/ .......... 64

Jedwali 21: Ubadala wa /ɲ/ > /j/ .......... 65

Jedwali 22: Ubadala wa /ʃ/ > /s/ .......... 65

Jedwali 23: Ubadala wa /f/ > /b/ .......... 66

Jedwali 24: Ubadala wa /v/ > /f/ .......... 66

Jedwali 25: Ubadala wa /g/ > /k/. .......... 67

Jedwali 26: Uchopekaji wa /j/ .......... 68

Jedwali 28: Uchopekaji wa /n/ .......... 69

Jedwali 29: Uchopekaji wa /h/ .......... 70

Jedwali 30: Kudhoofika kwa konsonanti /j/ hadi irabu /i/ .......... 70

Jedwali 31: Kudhoofika kwa /w/ hadi irabu /u/ .......... 71

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Kitangulizi

Katika sura hii tulilezea usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka na umuhimu wa utafiti.

## 1.2 Usuli wa Mada

Lugha zinapotagusana huwa na athari ambazo zinatokea kila upande. Athari hizi hazitokei tu kwa lugha katika makundi tofauti lakini pia katika lugha za kundi moja. Mbaabu (1985) anaeleza kuwa ujuzi wa lugha ya kwanza unaingiliana na Kiswahili. Maingiliano haya, ndio huleta athari na ni tatizo kubwa kwa wote wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili, kwa kuwa wana umilisi wa lugha moja. Richards (1974) anasema kuwa umilisi wa lugha ya kwanza ndio msingi wa kujifunza lugha ya pili. Anaeleza zaidi na kusema kuwa uzoefu wa matumizi ya lugha ya kwanza huhamishwa hadi lugha ya pili. Katika harakati za uhamisho huu, makosa hutokea kwa sababu fonolojia na mofolojia za lugha hizi mbili ni tofauti.

Basi ujifunzaji wa lugha ya pili utakuwa na shida na kutoa athari kubwa ikiwa lugha ya kwanza na lugha ya pili zinatofautiana kimuundo katika sauti. Na kama lugha hizi mbili zinatofauti kubwa, shida ya kujifunza lugha ya pili pia itakuwa kubwa. Ili kutambua shida za kujifunza lugha ya pili, tunafaa tuelewe tofauti kati ya lugha hizo mbili. Mbinu ya kuyatatua matatizo hayo ya athari ni kujua vile matatizo hayo yanavyojitokeza katika sauti, muundo wa maneno au hata sarufi.

Chimerah (2011), anasema kwamba lugha ya mama ni lugha ambayo mtu hujifunza kwa mara ya kwanza maishani mwake kabla ya lugha nyingine. Lugha ya pili ni lugha ambayo mtu alijifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Mtu huweza kujifunza lugha katika mazingira tofauti. Kwa mfano, anaweza kujifunza lugha hii kwa njia zisizo rasmi. Hii hufanyika kwa kuwasikiliza wenzake au kujifunza kirasmi darasani. Mtu pia anaweza kujifunza lugha ya pili kwa kuzingatia sera ya lugha katika nchi fulani.

Kimsingi, watafitiwa wenye umilisi katika lugha yao ya kwanza, huitegemea wakati wanapojifunza lugha ya pili. Kwa mujibu wa Richards (1974), tajriba ya mwanafunzi katika lugha ya kwanza huhamishwa katika lugha ya pili kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wake. Uhamishaji wa aina hii husababisha kuwapo kwa makosa mbalimbali hususani iwapo mifumo ya lugha mbili husika ni tofauti.

Chiraghdin na Mnyapala (1977) wanaeleza namna lugha ya Kiswahili ilivyoathiri na kuathiriwa na lugha zingine. Wanasema kuwa, "Kiswahili ni lugha ya watu walioko katika ukingo wa bara kubwa. Kwa hivo wenyeji wake hawana budi kuathiriwa na kuathiri watu wengine." Wameonyesha vile Kiarabu kilivyoathiri Kiswahili. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa lugha moja inaweza kuathiri nyingine panapokuwa na mtagusano.

Kiswahili kimepiga hatua kubwa sana kwa kupanuka zaidi na kuwa na majukumu si haba. Lengo likiwa kumudu mawasiliano ya kisasa katika nyanja zote za kitaaluma. Ni katika kutekeleza majukumu na pia kuathiri lugha za kiafrika na pia zisizo za kiafrika, licha ya kupanuka hivi na lugha hii kutwikwa majukumuhaya ndipo lugha ya Kiswahili imeathiriwa humu Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kati. Lugha hii imeigiliana na lugha zingine na kuathiriana.

Akichunguza athari za kimuundo kati ya lugha ya Kiswahili na Kitigania na kuzitolea maelezo ya kiisimu, Mukuthuria (2004) alisema kuwa utafiti wa athari, sio tu kutambua sababu za kuathiriana lakini pia, ni kutambua matatizo ya kiisimu yanayotokana na athari zinazoonyeshwa na utafiti wa aina hii, ili kuchunguza kama yanaweza kutatuliwa. Utafiti kuhusu athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili umewavutia wataalamu wengi lakini bado tafiti zaidi zinahitajika kubainisa chanzo cha athari ili kutuwezesha kuyatatua matatizo ya kujifunza Kiswahili.

Pia (1965) anasema kuwa watafiti Wataliano ambao walitafiti lugha ya Kisomali katika karne ya kumi na nane, walirejelea lugha hii kama ya Kikushiti neno ambalo lilitoka kwa Bibilia nchi ya Kushi . Baadaye watafiti waliofuata katika karne ya kumi na tisa waliita lugha ya pembe ya Afrika. Lugha ya Kisomali ni mojawapo wa lugha za Kikushiti kama Kiomoti, Kichad na

Kiberber (Saeed 1999). Lugha ya Kisomali inapatikana katika lugha za Kikushiti za mashariki pamoja na Kioromo, Kioromo ndiyo lugha iliyo na wazungumzaji wengi kuliko Kisomali (Mohamed 2013). Mohamed (2013) anaeleza zaidi kuwa, kuna watu zaidi ya milioni kumi na mbili ulimwenguni ambao lugha yao ya kwanza ni Kisomali. Lugha hii inazungumzwa sana na watu kutoka Somalia, sehemu nyingi za Djibouti, mashariki mwa Ethiopia na kwingineko ambako Wasomali wanakopatikana kama Ulaya, Australia na Merikani. Wasomali ndio watu wengi zaidi wanaoishi Minnesota kuliko jamii nyingine kutoka Afrika mashariki (Burke, 2001). Hapa nchini Kenya, lugha ya Kisomali huzungumzwa sehemu mbalimbali za Kitui, Mombasa, Nairobi, Migori, Isiolo, Kajiado, Namanga, Marsabit na zaidi maeneo ya kaskazini mashariki, ambayo yanajumuisha kaunti ya Wajir, Mandera na Garissa nchini Kenya. Lugha ya Kisomali katika kaunti hizi huzungumzwa na takriban asilimia tisini na tano ya waakazi katika maeneo haya (Mohamed 2013).

Mohamed (2013) anaelezea zaidi kuwa lahaja za lugha ya Kisomali zimewekwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza la lahaja ni Kimaxatiri, lahaja ambazo wasemaji wake wanapatikana kaskazini, magharibi na kusini mwa Somalia. Kundi la pili la lahaja ni Kibanadiri, wasemaji wa lahaja hizi wanaishi upwa wa Bahari Hindi na Mogadishu. Kundi la tatu la lahaja hizi ni Kimaay, wanaosema lahaja hizi ni Wasomali kutoka kusini magharibi mwa Somalia, sehemu za Kenya zinazopakana na Kenya katika upande wa kusini magharibi ambayo ni kaunti ya Garissa na upande wa mpaka wa Somalia na Ethiopia.

Kevogo na wenzake (2015) wakimnukuu (Lamberti 1986) wanasema lahaja za lugha ya Kisomali zinaainishwa katika makundi matano. Kundi la kwanza ni Kisomali cha kaskazini ambalo lenye lahaja ya Kikaskazini, lahaja ya Kidaarood, lahaja ya Kijuba cha chini. Kundi la pili ni Benaadir, ambalo lina lahaja ya Kiabgaal, Lahaja ya Kiajuraan, lahaja ya Kiaaljacal, lahaja ya Kixaman na lahaja ya Kibimaal. Kundi la tatu ni Ashraaf, ambalo lina lahaja ya Kishangaani na lahaja ya Kishebelle ya chini. Kundi la nne ni Maay na la tano ni Digil ambalo lina lahaja ya Kitunni, lahaja ya Kidabarre, lahaja ya Kigarre na lahaja ya Kijiiddu.

Lahaja ya Kidaarood ndiyo inatumika sehemu za kaskazini mashariki nchini Kenya (Kevogo na wenzake 2015).

Warsame (2001) anasema kuwa sheria ambayo inamtambulisha Msomali ni kuwa lugha yake ya kwanza ni Kisomali na anafuata utamaduni wa Kisomali. Lugha hii imepiga hatua kwa kuwa nchini Somalia imeteuliwa kuwa lugha ya kitaifa na mikakati ikawekwa, mojawapo ikiwa kuandikiwa vitabu vya kusoma, kufunzwa shuleni na kutumiwa kama lugha ya kufunzia masomo mengine huko Somalia (Bartoo, 2010).

Wasomali wanaopatikana sehemu hizi huingiliana na wale wa nchi jirani.Utafiti huu ulifanywa katika kaunti-ndogo ya Garissa-Township iliyo kaunti ya Garissa. Kufanya utafiti katika kaunti nzima data ingekuwa nyingi sana na ingechukua muda zaidi na gharama ya utafiti ingekuwa kubwa sana ambayo mtafiti hangeweza kukimu na utafiti kuchukua mda mrefu. Basi ikabidi mtafiti kufanya utafiti katika kaunti ndogo ya Garissa Township.

Utafiti huu ulihusu lugha ya Kisomali na ulichunguza athari za kimofofonolojia zinazotokana na lugha ya Kisomali miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Makosa hayo husababishwa na ujuzi wa lugha ya kwanza. Ili kubainisha athari ya Kisomali katika lugha ya Kiswahili sanifu utafiti wa aina hii ulihitajika ili kutambua matatizo ya kiisimu yanayotokana na athari za lugha ya Kisomali ili kuibua mikakati ya kuyatatua na kurahisisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Kiswahili ni lugha ya Afrika Mashariki na Kati iliyoenea na kujulikana na wengi zaidi katika maeneo haya kuliko lugha nyingineyo ya Afrika (Ali, 2010). Ni lugha ya Kibantu inayotumiwa kwa mawasiliano na sehemu za Afrika ya Kati na Mashariki. Bakari (1982) anaeleza kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi zaidi ya zote katika Afrika ya Kati na Mashariki. Iribe na Mukhwana (2011) na Okombo (2001) wanaitaja lugha ya Kiswahili kama lingua franka inayozungumzwa katika maeneo ya kusini mwa sahara barani Afrika. Aidha, ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na Tanzania.Vile vile ni moja kati ya lugha nne za taifa nchini Congo (Mwita, 2009).

Pia, Massamba (1990) anasawania na wataalamu hawa kwa kusema kuwa Kiswahili ni lingua franka katika Afrika ambapo kinatumiwa kama lugha ya pili na mamilioni ya watu hasa nchini Kenya, Tanzania,

Uganda, na hata Zaire Mashariki. Vile vile kunao wazungumzaji wa Kiswahili Burundi, Rwanda, Zambia na Malawi. Nchi hizi zote zinapatikana kusini mwa sahara, barani Afrika . Nchini Kenya lugha hii ni ya kitaifa na rasmi kwa mujibu wa katiba ya nchi iliyopitishwa mwaka wa elfu mbili na kumi. Somo la Kiswahili nchini hufunzwa kutoka shule za msingi hadi upili na kutahiniwa katika kiwango cha kitaifa kama somo la lazima. Na vilevile ni somo katika vyuo vya kadiri na vyuo vikuu nchini. Hapa nchini Kenya lugha hii inatumiwa katika nyanja si haba kama vile biashara, mtandaoni, uchukuzi na kwingineko. Nchini Tanzania lugha hii ndio hutolea mafunzo kwa wanafunzi katika shule za msingi.

Nchini Uganda Kiswahili ni lugha ya pili rasmi, Mukuthuria (2008). Kiswahili kikiteuliwa kuwa mojawapo ya lugha ya Muungano wa Afrika kutakifanya kikubalike katika mataifa mengi ya Afrika. Chimerah (2008), anasema, Kiswahili hufunzwa katika vyuo vingi Afrika na takribani vyuo mia kule Marekani. Hii ni ishara tosha kuwa lugha ya Kiswahili ni ya kimataifa. Musau na Chacha (2001) wakichangia umuhimu wa Kiswahili wanasema kuwa kuna matangazo ya redio kwa Kiswahili katika nchi tofauti kama vile Marekani (VOA), Uingereza (BBC), Ujerumani (Deutche welle) na kwingineko. Hivyo basi kwa kuchunguza matatizo ya athari ya lugha za kwanza katika Kiswahili na kuibua mbinu za kuyatatua kutarahisisha ujifunzaji wa Kiswahili na kuendeleza hadhi ya Kiswahili.

### 1.3 Swala la Utafiti

Kazi za wataalamu mbalimbali zimeonyesha kwamba aghalabu kuna athari za lugha ya kwanza katika matumizi ya lugha ya pili. Corder (1967) akizungumzia mwingiliano wa lugha na mapokezi na lugha ya pili, anaelezea kuwa makosa katika lugha ya pili yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyonayo mzungumzaji katika lugha ya pili kutokana na kuhamisha sifa fulani za lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Mutugu (2001) ameonyesha kuwa watumizi wengi wa Kiswahili kama L2 hukumbwa na matatizo katika matumizi yake kama L2. Makosa hayo hujitokeza katika viwango vya kifonolojia, mofolojia sintaksia na kadhalika.

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kisomali wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama L2. Wanapojifunza wanajipata wameandika au kusema tofauti na vile walivyokusudia basi wanatatiza uelewaji wa kile walichokikusudia kukisema, kwa hivyo ni muhimu kutambua makosa yako wapi na ni kanuni zipi zinazothibitisha makosa haya.

Aidha matokeo ya wanafunzi kutoka kaunti ya Garissa katika mitihani ya kitaifa katika somo la Kiswahili huwa duni. Tukiangazia kwa mfano matokeo ya mitihani ya miakaya 2015, 2016 na 2017 kulingana na ripoti rasmi ya Baraza la Mitihani ya Kitaifa ya Kenya, zaidi ya asilimia tisini ya wanafunzi waliofanya mitihani ya kitaifa hawakufikisha hata asilimia arobaini kwenye somo la Kiswahili.

Tafiti nyingi zimefanywa katika lugha mbalimbali zikionyesha vile umilisi wa lugha hizo unasababisha mtu kufanya makosa anapojifunza lugha ya Kiswahili au lugha nyingine kama L2. Tafiti hizo zimedhihirisha makosa yanajitokeza katika viwango mbalimbali vya isimu kama vile semantiki, fonolojia, mofofonolojia na kadhalika. Kulingana na ujuzi wetu, hakuna utafiti ambao umewahi kushughulikia makosa ya kimofofonolojia katika lugha ya Kisomali yanayojitokeza mwanafunzi msemaji Kisomali anapojifunza lugha ya Kiswahili kama L2 kutoka eneo la Garissa..

Basi utafiti huu unalenga kujaza pengo la usomaji isimu kwa kuonyesha makosa ya kimofofonolojia ambayo wanafunzi wasemaji wa Kisomali wanafanya wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama L2.

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni:

i) Kutambua makosa yanayojitokeza ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kisomali wanapojifunza Kiswahili.

ii) Kubainisha kanuni zinazodhibiti makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kisomali wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Ni makosa gani ya kimofofonolojia yanajitokeza wakati ambapo wanafunzi wazungumzaji wenyeji wa lugha ya Kisomali wanayafanya wanapojifunza lugha ya Kiswahili?

ii) Ni kanuni zipi zinazodhibiti makosa ya kimofofonolojia ambayo hufanywa na wanafunzi wa asili ya lugha ya Kisomali wanapojifunza lugha ya Kiswahili?

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulichunguza athari za lugha ya Kisomali ukizingatia lahaja ya Kidaarood ambayo hupatikana katika kaunti ndogo ya Garissa Township, kaunti ya Garissa. Athari hizi hufanyika katika ujifunzaji wa Kiswahili. Makosa yaliyoshughulikiwa ni ya kipengele cha kimofofonolojia ambacho kinahusu mofolojia na fonolojia ambavyo vikiunganishwa ni mofofonolojia na zinahusu sauti na uundaji wa maneno kutokana na sauti hizo. Umilisi wa sauti za lugha yoyote ni njia mwafaka ya kuelewa fonolojia ya lugha mahsusi. Taaluma zingine za isimu hazitashughulikiwa katika utafiti huu.

Utafiti huu uliwashirikisha wanafunzi kutoka shule sita za kutwa katika kaunti – ndogo ya Garissa Township katika kaunti ya Garissa. Kaunti hii inapatikana sehemu ya kaskazini mashariki mwa Kenya na sio kaunti ndogo zingine zinazopatikana katika kaunti hii. Wanafunzi walioshirikishwa ni wa kidato cha tatu ambao wanakisiwa kuwa wamepata umilisi wa kiwango

fulani katika lugha ya Kiswahili na wanaweza kujieleza ipasavyo kwa sababu wanafunzi hawa wana muda kwa kuwa hawatakuwa wanafanya mtihani wa kitaifa mwaka huo.

Utafiti huu haukushughulikia hatua mbili za mwisho katika nadharia ya uchanganuzi makosa ambazo ni kuonyesha athari zinazosababishwa na makosa hayo na jinsi ya kurekebisha makosa haya. Kwa kushughulikia hatua hizi utafiti huu ungekuwa mpana na ungechukua muda mwingi zaidi ikilinganishwa na muda uliotengewa shahada hii.

**1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ulisaidia kufahamu mfumo wa fonolojia ya lugha ya Kisomali ambao ni ujuzi muhimu katika usomaji wa isimu. Ufahamu huu unasaidia kuimarisha matamshi bora ya sauti na kwa hivyo kuimarisha matumizi ya lugha fasaha. Pili, huweka misingi ya jinsi lugha tofauti zinavyotumia sauti chache tu ili kuunda maneno.

Utafiti huu ulionyesha mifanyiko ya kimofofonolojia na kanuni zinazoongoza athari zinazofanywa na msemaji wa lugha ya Kisomali katika lugha ya Kiswahili ambao ni mchango mkubwa katika uwanja wa isimu za lugha za Kiafrika.

Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama kirejelewa kwa watafiti wa baadaye. Utafiti huu unatoa mchango kwa wasomi wa Kiswahili kwani ni tafiti chache zimefanywa kuhusu uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia za lugha ya Kikushiti katika lugha ya Kiswahili. Umeweza kuongeza ujuzi wa kiisimu wa lugha za Kiafrika hasa lugha za kaskazini na mashariki ya Kenya.

Utafiti huu unasaidia wasemaji wa Kisomali katika kuelewa Kiswahili na kurahisisha mawasiliano kati ya wanafunzi, wahudumu, walimu, ama kwa mtu mwingine yeyote, kwani lugha ya Kiswahili ni ya kitaifa.

Utafiti huu ulidhihirisha athari za kimofofonolojia katika lugha ya pili. Ujuzi ambao umepatikana katika utafiti huu utasaidia katika kupunguza athari hii, kwa kuweka wazi kanuni

ambazo zinazohusu mofofonolojia. Utofauti katika fonolojia za lugha hizi mbili tunatarajia msomi wa lugha ya pili aweze kufanya makosa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Kitangulizi

Katika sura hii tulielezea maandiko mbalimbali aliyoyapitia yanayohusiana na mada hii, misingi ya kinadharia iliyotuongoza katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Dhana ya mofolojia, dhana ya mofofonolojia, dhana ya fonimu, dhana ya mofimu , fonolojia ya Kiswahili na fonolojia ya Kisomali zimeelezewa katika sura hii.

## 2.2 Misingi ya Nadharia

Utafitihuu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (N.U.M). Nadharia hii iliasisiwa na Corder mnamo mwaka wa 1967. Nadharia hii inachunguza makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha ya pili (Gas na Selinker 2008). Uchanganuzi Makosa hutumiwa kuthibitisha makosa yanayopatikana mwanafunzi anapojifunza lugha. Walimu wa lugha wanaowasikiliza wanafunzi wao wakizungumza hutambua makosa hayo. Ukweli ni kuwa kila mtu hufanya makosa anapoongea hata walimu na wazawa wa lugha hufanya makosa.

Uchanganuzi Makosa huchunguza aina ya makosa na visababishi vya makosa hayo. Corder (1967) ameonyesha misingi ya N.U.M kama ifuatayo:

i) Katika ujifunzaji wa L2, mwanafunzi lazima afanye makosa.

ii) Kufanya makosa ni kawaida kwa hivyo mwanafunzi anapofanya makosa asiadhibiwe bali makosa hayo yachukuliwe kama kigezo cha kuthibitisha kuwa bado hajajifundisha lugha.

Kwa hivyo hatua zifuatazo zitekelezwe;

a) Makosa yaweze kutambulika

b) Makosa hayo yaainishwe

c) Njia mwafaka za kurekebisha makosa hayo ziweze kupendekezwa

Kulingana na mwanaisimu Corder (1967), mtafiti anapaswa kufuata hatua zifuatazo katika uchanganuzi wa makosa:

i) Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha ya pili. Kwa mfano kukusanya insha za wanafunzi wa kidato cha tatu ambazo wameandika kutoka na mada ambayo tulikuwa tumewateulia.

ii) Kutambua makosa. Kwa mfano uchopekaji wa fonimu katika uundaji wa maneno, Ubadilishaji wa fonimu wakati mwanafunzi anapounda maneno ya Kiswahili na udondoshaji wa fonimu fulani katika uundaji wa maneno.

iii) Kueleza makosa, katika hatua hii makosa yanawekwa katika makundi na kuelezwa kisarufi. Hivyo makosa yenyewe ndiyo hutumiwa katika kuainisha kategoria za kisarufi.

iv) Kuhesabu makosa. Katika hatua hii idadi ya makosa katika kila kundi hutambuliwa.

v) Kutambua vipengele vyenye matatizo. Vipengele vya lugha vinavyowatatiza wanafunzi na kusababisha makosa hutambuliwa. Kwa mfano, fonimu fulani, virejeshi, vitenzi, nyakati, miundo ya silabi na kadhalika.

vi) Kufafanua chanzo cha makosa haya. Kwa mfano athari ya lugha ya kwanza ya Kisomali mwanafunzi anapojifunza lugha ya Kiswahili kama L2. Ukosefu wa mazoezi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa mwanafunzi.

vii) Kuyasahihisha makosa hayo ili kujua jinsi ya kukabiliana na makosa. Kwa mfano mwanafunzi kuwa na jedwali au chati ya kuonyesha makosa anayofanya na jinsi ya kuyarekebisha.

Tunapowasikia wanafunzi wakizungumza tunafahamu makosa wanayofanya. Basi ni vyema kujiuliza kile mzungumzaji alikusudia kukisema na angesema vipi. Kusahihisha makosa kunategemea kile msikilizaji anafikiri mzungumzaji alikusudia kukisema na kosa lenyewe. Ni vyema kufikiri namna nyingi tofauti za kusahihisha makosa, kwa sababu

hakuna uhakika wa kilichokusudiwa kuwasilishwa, mwanafunzi anapaswa kushirikishwa katika kuamua jibu sahihi.

viii) Kuonyesha athari inayosababishwa na makosa hayo. Baadhi ya athari zinazotokana na makosa haya ni kutatanisha mawasiliano, kuanguka mtihani na kadhalika.

Ili kufafanua makosa haya yafaa kujua kisababishi. Makosa yanaweza kutokana na kuhamisha kanuni au ruwaza za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Makosa mengine yanaweza kusababishwa na jinsi mwalimu alivyoeleza kanuni fulani.

## 2.3 Mapitio ya kazi Mbalimbali

Cozby na Bates (2012), wanaeleza kwamba mapitio ya maandiko ni nakala zote zilizoelezea kwa ufupi tafiti zilizokwisha fanyika katika eneo fulani. Kupitia maandiko ni mchango unaohusu uchunguzi wa kina kwa maandiko yaliyotangulia eneo fulani la taaluma. Kazi hizi zinaweza kuwa vitabu, makala au majarida.

Lengo la kusoma mapitio ya kazi nikuchambua tafiti ili kubaini pengo lililopo, ili kumpa mtafiti changamoto ya kutaka kuziba pengo la kitaaluma linalohitaji kujazwa kikamilifu au kwa kiasi fulani. Mapitio ya kazi mbalimbali hutoa mwongozo kwa mtafiti. Mchango mzima wa upitiaji wa kazi mbalimbali hufungamana na kanuni zake kama kuhakiki, kujadili na kutoa maoni ya utafiti ili kuboresha utafiti unaokusudiwa kufanywa. Hivyo, utafiti huu unaendelea na kazi zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali.

### 2.3.1 Makosa yanayojitokeza mwanafunzi anapojifunza lugha ya Kiswahili

Mhilu (2005), anasema kwamba lugha ya mama hutumika katika shughuli za mawasiliano ya kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii. Lugha ilisaidia watu kuelewana wao kwa wao na kuwawezesha katika shughuli zao za kiuchumi na kiutamaduni kwa jamii husika, ambayo ni tofauti na kutumia lugha zaidi ya moja. Anaendelea kufafanua kuwa matumizi ya lugha zaidi ya moja husababisha utata katika jamii na hatimaye kudidimiza maendeleo. Mfano ni mataifa

kama: Japani, China na Ufaransa yaliyoendelea kutokana na matumizi mkubwa wa lugha ya mama.

Mwakaryz (2011), alichunguza athari za matumizi ya lugha ya Sheng katika lugha ya Kiswahili. Kazi yake ilidhiirisha kuwepo na athari mbalimbali za kimatamshi katika lugha ya Sheng. Utafiti wa Mwakaryz ulihusu kipengele cha fonolojia ambacho ni kiambajengo cha kipengele cha mofofonolojia, basi yeye hakutafiti kipengele cha mofolojia pengo ambalo utafiti huu unalenga kuziba.Utafiti ulihusu athari ya lugha ya Kisomali katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Sampuli tuliotumia ilikuwa wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka shule za upili za kutwa, kaunti ndogo ya Garissa Township.

Musau (1993) aliendeleza utafiti wake katika fonolojia ya Kiswahili na kushughulikia makundi ya lugha yafuatayo: Kinandi, Kikamba, Kikuyu, Kibukusu, Kisomali, Kimaasai na Kiluo. Sampuli yake ilikuwa ni wanafunzi katika vyuo vya walimu wa shule za msingi ambavyo ni Thogoto, Highridge na Machakos. Katika utafiti wake aliainisha jinsi wazungumzaji wa lugha hizi wanavyoathiriwa na lugha zao za kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti wake ulikuwa muhimu sana katika kuwekea msingi tafiti za baadaye. Mchango wake mkubwa katika utafiti wake ni pale anapozugumzia matamshi. Anasema kuwa jambo muhimu ambalo linasaidia utamkaji bora ni mwanafunzi kuelewa sauti anazopaswa kutamka. Mwalimu anapaswa kuelewa vyema mahali pa kutamkia sauti mbalimbali na ala za matamshi zinazohusika ili kuweza kumsaidia mwanafunzi.

Musau anaangalia sampuli nyingi za lugha, kwa hivyo hakueleza kila moja kwa kina. Hakuzuru maeneo ya lugha hizo zinakotumika bali katika vyuo, akasasahau kuwa kuna mambo mengi ambayo yanaathiri matumizi ya lugha.Utafiti wake uliacha pengo, kwani ulijikita katika fonolojia na haukushughulikia athari ya kimofofonolojia. Lakini utafiti tuliofanya ulihusu wanafunzi wa Kisomali huko mashinani.

Mbaabu (1995) alishughulikia makosa yanayojitokeza katika Kiswahili. Anayaainisha makosa yanayofanywa katika makundi manne ambayo ni kundi la kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi. Makundi haya manne huingiliana kiasi kwamba kosa la kimatamshi linaweza pia kuwa la kisarufi na linaweza kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Mbaabu anatambua kuwa makosa mengi ya kimatamshi yanatokana na maingiliano ya lugha ya kwanza katika Kiswahili sanifu. Alitumia mifano kadhaa kutoka lugha nyingi za kwanza na kuangilia makosa yanayohusu sauti. Makosa yanayohusu upatanifu katika ngeli za nomino na makosa yanayohusu sentensi. Utafiti wake ulikuwa na mchango sana katika utafiti huu kwa kuwa katika kushughulikia makosa ya kifonolojia ni lazima tuzigatie makosa yanayohusu sauti. Utafiti wetu utahusu kiwango cha kimofofonolojia. Utafiti wake ulishughulikia masuala mengi ya lugha na haukulenga lugha moja maalum ili kuishughulikia kwa kina zaidi kama tulivyojadili katika lugha ya Kisomali. Pili utafiti wetu utawahusu wanafunzi wa Kisomali katika maeneo ya mashinani ambao ni wazungumzaji asilia wa lugha ya Kisomali. Lakini utafiti wake uliwahusu wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu ambao huenda wakawa na athari zingine za kimazingira.

Cross (2009) alifanya utafiti wake kwa wanafunzi wa Kijapan wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa wanafunzi waliathirika na lugha yao ya kwanza. Walikuwa na shida katika kutofautisha sauti /b/ na /v/, waliziunganisha sauti hizi mbili na kuzitamka kama /v/ ya Kijapan.

Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha pia kuwa wanafunzi walikuwa na shida ya kutofautisha kati ya sauti /l/ na /r/ kwa sababu Kijapani hakina konsonanti hizi mbili bali kina fonimu /r/ ambayo hutokea katikati ya hizi konsonanti mbili za Kiingereza. Katika utafiti wake pia wanafunzi wengi walibadilisha fonimu ya Kiingereza /l/ na /r/ aghalabu kwa kuiona ikikaribiana sana na ile /r/ ya Kijapan. Cross alishughulikia kipengele cha fonolojia. Utafiti wake ulionyesha kuwa kuna haja ya kushughulikia athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji ya lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Utafiti tuliofanya ulihusu kipengele cha kimofofonolojia, ambacho kinachangiwa na fonolojia.

Kanake (2013) alifanya utafiti wake kwa kuzingatia athari ya lugha ya Kiigembe, mojawapo ya lahaja za Kimeru, katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wasemaji wanaojifunza lugha ya Kiswahili.  Alibaini kuwa wanafunzi walifanya makosa wanapotumia lugha ya Kiswahili hasa katika kiwango cha kifonolojia kwa kuhamisha mfumo wa Kiigembe katika Kiswahili. Utafiti wetu ni tofauti na wake kwa kuwa yeye ameshughulika lahaja ya Kiigembe ambayo ni ya Kibantu ilhali utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kisomali ambayo ni Kikushitiki tukizingatia lahaja ya Kidaarood.

Kevogo (2007), alishughulikia makosa ya kisarufi na jinsi yanavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Alichunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa darasa la nane miongoni mwa jamii ya Wadholuo. Katika utafiti wake aligundua kwamba lugha ya kwanza ya wanafunzi iliathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Kevogo alishughulikia athari ya kisarufi kwa hivyo hakujihusisha na kipengele kingine cha isimu, kwa hivo kulikuwa na haja ya kushughulikia athari katika viwango hivi. Jambo ambalo utafiti huu ulilenga kuziba katika kiwango cha kimofofonolojia ukizingatia wasemaji wa lugha ya Kisomali ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Lugha ya kwanza aliyoishughulikia ni Kidholuo kutoka wilaya ya Bondo. Nao utafiti huu ulitumia lugha ya kwanza ya Kisomali kutoka kaunti-ndogo ya Garissa-Township. Pili utafiti wake uliwashirikisha wanafunzi wasemaji wa Kidholuo wa darasa la nane kutoka shule za msingi ilhali utafiti huu ulishirikisha wanafunzi wasemaji wa Kisomali wa kidato cha tatu kutika shule za upili.

Musa (2008), alichunguza athari za lugha ya Kigweno katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na jinsi zinavyoathiri matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne. Katika kuchanganua data Musa alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ikisaidiwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Musa alishughulikia vipengele vya kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia. Data iliyokusanywa ilitokana na mazungumzo ya wanafunzi katika mijadala. Katika utafiti wake aligundua kwamba athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili huathiri matokeo ya mtihani kwa kiwango kikubwa. Utafiti wa Musa ulitofautiana na

huu, kwa sababu tulishughulikia lugha ya Kisomali ambayo iko kundi la Kushitiki naye Musa alitafiti lugha ya Kigweno ambayo iko katika kundi la Kibantu. Pili Musa alishirikisha wanafunzi wasemaji wa Kigweno wa kidato cha nne nami nilishirikisha wanafunzi wasemaji wa Kisomali wa kidato cha tatu. Tatu Musa alishughulikia vipengele vya semantiki, mofolojia na sintaksia lakini utafiti huu ulishughulikia kipengele cha kimofofonolojia.

Ng'ang'a (2002), alifanya utafiti kuhusu makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa darasa la saba na jinsi yanavyoshughulikiwa na walimu katika tarafa ya Ndaragwa. Alichunguza makosa ya kisintaksia, kisemantiki, kimofolojia na hijai. Lugha ya kwanza ya wanafunzi ilikuwa Kikikuyu na lugha ya pili ya wanafunzi wasemaji wa Kikuyu ilikuwa Kiingereza. Data ilikusanywa kutokana na insha za lugha ya Kiingereza kutoka kwa wanafunzi wa darasa la saba. Alibaini kuwa lugha ya Kiingereza iliathiriwa na Kikuyu kwani makosa mengi yaliyobainika yalisababishwa na athari za lugha ya kwanza.

Utafiti wa Ng'ang'a ulitofautiana na tulioufanya kwa sababu yeye alishughulikia athari ya Kikuyu kwa Kiingereza ambayo ni lugha yao ya pili. Ilhali utafiti huu ulichanganua makosa ya kimofofonolojia ambayo yanafanywa na wanafunzi wasemaji wa Kisomali ambao lugha yao ya kwanza ni Kisomali na wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ng'ang'a alichunguza makosa ya kisemantiki, kimofolojia, kisintaksia na hijai. Lakini utafiti huu utahusu kipengele cha kimofofonolojia. Mwisho, Ng'ang'a alishirikisha wanafunzi wasemaji wa Kikuyu wa darasa la saba kutoka wilaya ya Ndaragwa ilhali utafiti huu uliwashirikisha wanafunzi wasemaji wa Kisomali wa kidato cha tatu kutoka kaunti-ndogo ya Garissa-Township.

Kitsao (2015) alitafiti kuhusu makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika kata ya Ganze. Alishughulikia vipengele vya sintaksia na mofolojia ambavyo muungano wake ni mofosintaksia. Utafiti wake uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Lugha ya washiriki ilikuwa Kigiriama na lugha ya pili ilikuwa Kiswahili ambayo walikuwa wakijifunza. Data iliyokusanywa ilitokana na insha za lugha ya Kiswahili ambazo zilikuwa zimeandikwa na wanafunzi wa darasa la nane. Alibaini

kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa na lugha ya Kigiriama. Kwani, makosa mengi yaliyobainika yalisababishwa na athari za lugha ya kwanza. Utafiti huu utatofautiana na wa Kitsao kwa namna mbalimbali. Kwanza, Kitsao alishughulikia athari ya lugha ya kwanza ya Kigiriama katika kipengele cha mofosintaksia lakini utafiti huu ulishughulikia athari ya lugha ya Kisomali katika kipengele cha kimofofonolojia. Pili, alishirikisha wanafunzi wa darasa la nane kutoka kata ya Ganze lakini utafiti tuliofanya uliwashirikisha wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka kaunti-ndogo ya Garissa-Township. Tatu lugha ya Kigiriama ambayo imetumiwa kama L1 iko katika kundi la Kibantu ilhali lugha ya Kisomali tulichotumia kama L1 iko katika kundi la Kikushitiki.

Otiende(2013) alichunguza athari ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili. Alijishughulisha na kipengele cha kimofofonolojia. Kwa hivyo, makosa ambayo alikuwa akichanganua yalikuwa ya kimofofonolojia. Katika utafiti wake alitumia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Mtafiti aliwashirikisha wanafunzi wa darasa la nne, sita, na nane kutoka shule za msingi ambazo zinapatikana katika kisiwa cha Mfangamano.

Wanafunzi hawa walikuwa katika wasemaji asilia wa Kiolusuba. Data iliyotumiwa katika utafiti huu ilipatikana kupitia mbinu ya mahojiano na uandishi wa insha. Utafiti wa Otiende ulitofautiana na huu tuliofanya kwa kuwa, kwanza, alijishughulisha na athari ya lugha ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili. Basi L1 ni Kiolusuba na L2 ni Kiswahili.

Uchanganuzi wake ulihusu kipengele cha kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kiolusuba wa darasa la nne ilhali utafiti tuliofanya ulishughukia wanafunzi wasemaji wa Kisomali wanapojifunza Kiswahili. Basi L1 ni Kisomali na L2 ni Kiswahili. Pili, alishirikisha wanafunzi wa darasa la nne, sita na nane kutoka shule za msingi za eneo la Ziwa Victoria lakini tulioufanya ulishirikisha wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka kaunti-ndogo ya Garissa-Township. Tatu, utafiti wake umetumia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilhali huu ulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Tafiti zote zimekuwa hazina kubwa katika usomaji wa isimu.

Were (1994) alitafiti kuhusu athari zinazotokana na L1 zinazodhihirika katika uandishi wa insha za Kiswahili. Yeye alishughulikia makosa ya kimsamiati, tahajia na sarufi. Katika utafiti wake alitambua kuwa kuna ile hali ya wanafunzi kujumlisha sheria na pia kuzihamisha kutoka L1 hadi L2 ambayo ni Kiswahili.

Utafiti huu unatofautiana na tuliofanya kwa namna ifuatayo; alishughulikia makosa ya kimsamiati, tahajia na sarufi ilhali tulioufanya ulihusu kipengele cha kimofofonolojia. Were alishughulikia lugha ya Kiolusuba kama L1 lakini utafiti tuliyofanya ulishughulikia lugha ya Kisomali kama L1.

Rapando (2005) alichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Alishughulikia wanafunzi walio na asili anuwai ambao huenda hawana makosa ya sampuli ya kutabirika kwa kuwa baadhi ya makosa aliyoyashughulikia yanatokana na Kiingereza na ‘Sheng’ ambayo ni lugha kipindi inayobadilika kila mara. Aidha baadhi yao wanaathirika na L1 ya wazazi wao. Utafiti wa Rapando unatofautiana na huu tuliyofanya kwa kuwa utafiti wake haukuwa na kundi mahususi kwani wanaotumia lugha ya Sheng huwa ni watu kutoka jamii tofauti tofauti ambazo zina lugha zao. Basi wasemaji wa Sheng watakuwa wanatumia lugha ya Kiingereza kama lugha yao ya tatu ambayo ingeweza kuchunguzwa na matokeo kujumlishwa, lakini utafiti huu ulikuwa na kundi mahususi ambalo lilitambulishwa na lugha ya Kisomali na pia ni wanafunzi wa kidato cha tatu.

Mutugu (2001) alichunguza makosa ya kileksia kutoka kwa lugha ya Kikuyu ambayo yaliathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti wake ulifanyika katika wilaya ya Kiambu na kushirikisha wanafunzi wa kidato cha pili ambao waliandika insha. Mutugu alingawanya wilaya hii katika sehumu tano na kila sehemu iliwakilishwa na shule moja kwa hivyo, alikuwa na shule tano. Lakini utafiti wa Mutugu ni tofauti na tuliyofanya, kwanza, tulishirikisha wanafunzi wasemaji wa Kisomali wa kidato cha tatu kutoka kaunti ndogo ya Garissa Township. Pili, tulishughulikia makosa ya kimofofonolojia, data ambayo tulipata tukitumia vifaa vya insha na hadithi.

Chepkwony (2011) alichunguza makosa ya mofosintaksia miongoni mwa Wakipsigis wanayofanya katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Sampuli aliyotumia ilitoka katika shule za msingi katika wilaya ya Bomet ambapo alishirikisha wanafunzi wa darasa la sita, saba na nane kutoka shule nne.

Makosa ya mofosintaksia aliyoshughulikia yalikuwa miundo ya maneno, virai, vishazi, nomino-vimilikishi, nomino-vivumishi vya sifa na nomino-vivumishi vya idadi. Utafiti tuliyofanya ulishughulikia makosa ya kimofofonolojia yaliyofanywa na wanafunzi wasemaji wa lugha ya Kisomali kutoka kaunti ndogo ya Garissa Township. Lugha za Kikipsigis na Kisomali zimetoka katika lugha mame tofauti na lugha ya Kiswahili.

Evans (2011) ametafiti kuhusu ukopaji katika lugha ya Kibukusu. Utafiti wake umezingatia michakato ya kimofofonolojia ambayo inahusiana na mofolojia katika mageuzi ya maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza hadi Lubukusu. Ameonyesha uhusiano uliopo katika fonolojia na mofolojia katika mageuzi ya maumbo yenye mantiki yanayokopwa.

Evans (2011) ameweza kubainisha kanuni zinazoongoza mageuzi ya kimofofonolojia ya maneno-mkopo ya lugha ya Kibukusu. Evans (2011) ametumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia katika kuchanganua maneno-mkopo ya lugha ya Kibukusu.

Utafiti wa Evans (2011) ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwa jinsi ambavyo umetoa mwangaza wa michakato ya kifonolojia inayopitiwa na maneno yanayokopwa na lugha ya Kibukusu kutoka lugha ya Kiingereza na jinsi ya kubainisha kanuni za michakato hiyo. Tofauti ya utafiti wa Evans (2011) na utafiti huu tumefanya ni kwamba lugha ambazo zimechanganuliwa ni tofauti; utafiti wa Evans (2011) umezingatia Kiingereza na Lubukusu ilhali utafiti huu unahusisha lugha ya Kisomali na Kiswahili. Pili ulibainisha michakato ya kimofofonolojia ambayo maneno ya Kiswahili yanapotamkwa na msemaji wa Kisomali yanapitia ili kudhihirisha athari. Tatu utafiti huu umetumia nadharia ya uchanganunzi makosa.

Conway (2008) alishughulikia utamkaji wa fonimu sita za lugha ya Kisomali vile zinavyoathiri hujifunzaji wa Kiingereza kama lugha ya pili. Conway alikusudia kubaini sifa ambazo zingemfanya msemaji wa Kiingereza kumuelewa msemaji wa Kisomali.

Alifanya utafiti wake katika jimbo la Minnesota, nchini Marekani ambako kuna wasemaji wa lugha ya Kisomali. Watu hawa walikuwa wanajifunza lugha ya Kiingereza kama lugha yao ya pili na ilikuwa inatumika kufunzia huko Minnesota. Utafiti wa Conway ulitofautiana na tuliyoufanya kwa kiwango kikubwa. Kwanza, sampuli aliyotumia ni wanafunzi wasemaji wa lugha ya Kisomali wanaoishi jimbo la Minnesota ambao walikuwa wanajifunza lugha ya Kiiingereza.

Wasomali hawa walipokuwa wakihamia huko hawakuzingatia lahaja ambazo zilitumika Somalia kwani walikuwa katika pilkapilka za kwenda mafichoni kwa hivyo, Conway hakuzingatia lahaja lakini utafiti tuliyoufanya uliangazia Wasomali wa Kenya na hasa wenye lahaja ya Kidaarod ambayo hupatikana kaunti ya Garissa. Wasemaji wa lugha ya Kisomali walikuwa wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Utafiti wetu uliangazia fonimu zote za lugha ya Kisomali na vile zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Conway hakuzingatia kuwa mbali na lugha ya kwanza kuna mambo mengine ambayo yanaweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Mambo kama vile saikolojia na mazingira geni.

Mwita (2014) alitafiti makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayoibuka katika kazi za wanafunzi waliokuwa wakijifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili na lugha za kwanza zilikuwa Kikuria na Kidholuo. Alishirikisha wanafunzi wa darasa la nane.

Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Ulinganuzi Makosa ambayo iliasisiwa na Lado (1957). Katika nadharia hii anadai kuwa miundo ya kiisimu inayofanana baina L1 na L2 inakuwa ni rahisi kujifunza ilhali miundo na mifumo tofauti huwa migumu kujifunza.

Pia, alitumia nadharia ya Corder (1967,1981) ambayo inasema kwamba watu wanapojifunza lugha ya pili huwa na athari ya lugha ya kwanza na huhamisha kanuni za lugha ya kwanza

hadi lugha ya pili. Utafiti huu tuliofanya umeshirikisha wanafunzi wa kidato cha tatu wasemaji wa lugha ya Kisomali.

Kisakwah (2014) alichanganua makosa ya kisintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kilosuba wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Data yake ilikuwa ni sentensi ambazo alizilinganisha kimuundo, sentensi sahili ya Kilosuba na muundo wa sentensi ya Kiswahili. Data hii alipata kutoka kwa tungo wanafunzi wasemaji wa Kilosuba waliandika, kisha alibaini kiwango cha uhawilishaji wa Kilosuba hadi Kiswahili sanifu.

Ili kuafikia haya aliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi tofauti na utafiti tuliyofanya ambao umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Wasemaji tuliotafiti lugha yao ya kwanza ilikuwa Kisomali ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulijishughulisha na makosa ya kimofofonolojia.

Otiende (2013) alichunguza athari za kimofolojia za Kilosuba katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulidhihirisha kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kilosuba ambao huathiri matumizi ya Kiswahili. Aidha, alishughulikia swala la athari za lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili. Utafiti huu ulitufaa kwani tumebaini kuwa na haja ya kushughulikia matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.
Mudhune (1994) alichunguza iwapo tofauti za kategoria za kisarufi kati ya Kiswahili na Kiluo zinaweza kusababisha matatizo kwa msemaji wa Kiluo wanapojifunza Kiswahili sanifu. Utafiti wake ulifanywa kwa wanafunzi wa darasa la sita, kutoka shule nne wilayani Siaya, alibaini kuwa matatizo mengi yanatokana na athari za lugha ya kwanza yaani Kiluo.
Makosa mengine hutokana na ujumlishaji mno wa kanuni za ngeli ya tisa ya Kiswahili, hii ni kwa sababu ngeli ya tisa ina majina mengi kuliko ngeli zingine na vilevile huwa na sifa za kipekee. Kwa mfano tofauti ya umoja na wingi katika ngeli hii hueleweka kwa urahisi kuliko ngeli zingine. Aidha yaonekana kuwa wanafunzi hutumia ngeli hii mara kwa mara labda kutokana na usahili wake utafiti huu ulifanywa kwa wanafunzi wa darasa la sita.

Utafiti wa Mudhune ulihusiana na ule tulioufanya kwa kuwa mwanaisimu hawezi kuzungumzia kipengele cha kisintaksia kabla ya kujadili kifonolojia na kimofolojia, kwani viwango huchangia katika kuunda maneno ambayo yalitumiwa katika sintaksia.

Utafiti wa Mudhune ni tofauti na ule tumefanya kwa sababu yeye alichunguza iwapo tofauti za kategoria za kisarufi kati ya Kiswahili na Kiluo zinaweza kusababisha matatizo kwa wasemaji wa Kiluo wanapojifunza Kiswahili. Mudhune aliacha pengo la kiisimu katika kiwango cha kimofofonolojia ambalo tulilijaza, kwa kutafitia kuhusu athari za lugha ya Kisomali unapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Mekacha (2011), alieleza kuwa lugha ya Kiswahili inafanana na lugha zingine za Kibantu kwa kudai kwamba, lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyotokana na uhusiano wa lugha zingine za Kibantu. Kwa mfano**,** wataalamu maarufu wamedhihirisha kwamba lugha ya Kiswahili inafanana na zile za Kibantu katika mfululizo wa msamiati wa msingi ya vitu vya kawaida na vya asili katika mazingira. Kazi hii ilidhihirisha kuwa lugha zinaweza kuathiriana na hata kupelekea kuzaliwa kwa lugha mpya.

He Dan (2010), alitafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Kichina wanapojifunza Kiingereza kama L2, lugha yao ya kwanza ikiwa Kichina katika Chuo Kikuu cha Huizho. Alitumia Nadharia ya Mwingiliano lugha ambapo alizingatia makosa yanayotokana na uhamishaji wa Kichina kwa Kiingereza vilevile makosa ya kisintaksia. Data aliyokusanywa ilitoka kwa insha za wanafunzi. Utafiti wa He Dan unawiana na ule tumefanya kwa sababu sote tunachunguza makosa ya yanayofanywa na wanafunzi wanapotumia lugha ya pili. Utafiti wa He Dan hauwezi kamilika iwapo hakuna sauti na sauti hizo kuunda maneno, kwa hivyo utatifi huu umejishughulisha na kimofofonolojia. Ilhali kuna tofauti kadhaa; kwanza, He Dan alifanya utafiti wake nchini China katika Chuo kikuu, lugha ya kwanza ikiwa Kichina na pili ikiwa ni Kiingereza. Makosa aliyoshughulikia yalikuwa ya kisintaksia na kisemantiki.

Utafiti huu tulifanya katika shule za upili za umma kutoka kaunti-ndogo ya Garissa-Township, kaunti ya Garissa, nchini Kenya. Na tulishughulikia makosa ya kimofofonolojia. Lugha ya kwanza ikiwa kisomali na lugha ya pili ikiwa Kiswahili.

Yule (2010), alisema kwamba matamshi ya utamkaji wa sauti ya binadamu huzingatia muktadha au mazingira ya mazungumzo. Athari ambazo hujitokeza kwa wazugumzaji wa lugha ya pili, zinajitokeza kwa kuwa na utofauti wa utamkaji wa maneno ya Kiswahili na tofauti hizo hujitokeza katika matamshi na lafudhi kwa mzungumzaji wa Kiswahili.

Onyango (1997) alishungulikia uziada wa kisarufi katika wanafunzi wa Kinyala, alilenga kubainisha iwapo tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili sanifu zinasababisha athari katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Alibaini kuwa makosa mengi ya wanafunzi husababishwa na athari za lugha ya kwanza. Hata hivyo kuna makosa mengine ambayo hayahusiani na athari. Athari za lugha ya kwanza zinatokana na upunguzaji uziada. Utafiti wake ulionyesha kuwa idadi kubwa ya makosa ilihusu kategoria ya virejeshi ikifuatwa na nafsi, kisha tarakimu. Utafiti huu aidha ulifanywa kwa wanafunzi wa darasa la nane kutoka shule nne za msingi wilayani Busia. Onyango alishugulikia uziada kwa wanafunzi wa Kinyala wa darasa la nane waliokuwa wanajifunza Kiswahili. Utafiti wa Onyango unahusu lugha tofauti ambayo ni Kinyala lakini huu ulihusu lugha ya Kisomali na makosa ya kimofofonolojia kwa wanafunzi wa shule ya upili waliokuwa wanajifunza lugha ya Kiswahili.

.Lakkis na Malak (2000 ) walichunguza uhamishaji wa ujuzi kuhusu vihusishi uliofanywa na wanafunzi wa Kiarabu kutoka lugha ya Kiarabu kuhusishana lugha ya Kiingereza. Walizingatia uhamishaji chanya na hasi ili kuwasaidia walimu kutambua vipengele tata. Ugunduzi huu ungesaidia kuwaelekeza wanafunzi husika kuhusu wakati wakutumia uhamishaji na wakati wakutoutumia. Walihitimisha kuwa mwalimu ambaye lugha yake ya kwanza ilikuwa Kiarabu, alikuwa katika nafasi nzuri ya kutumia miundo ya vihusishi katika Kiarabu pale ambapo miundo hiyo iliafikiana na ile ya Kiingereza.

Aidha,walimu husika walikuwa na wajibu wa kuwaonesha wanafunzi wao kuwa vitenzi na semi nyingine huambatishwa na vihusishi kwa njia isiyoafikiana na miundo ya lugha yao ya kwanza.

Kulingana na Mbaabu (1995) na King'ei na Musau (2000) matatizo ya matamshi husababishwa na athari za lugha za kimsingi. Hivi ni kumaanisha kuwa umilisi wa lugha ya kwanza katika matamshi itapelekea makosa ya kifonolojia pale ambapo mtu anajaribu kujifunza lugha ya pili. Vilevile aina za makosa ya kimaendelezo ambayo hutokea hudhihirisha hizo athari za kimatamshi.

Bartoo (2004), akichunguza kuhusu ujifunzaji wa sintaksia ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaotumia Kikeiyo kama lugha ya kwanza, aligundua kuwa Kikeiyo kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiingereza. Anasema kwamba, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizo mbili, wanafunzi husika walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao hadi katika lugha ya Kiingereza. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyoyabainisha mtafiti huyu katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa hao. Bartoo hakushughulikia sauti ambazo ni muhimu katika usomaji wa lugha yeyote ile, kwanza angejishughulisha na kipengele cha fonolojia.

Akishughulikia kuibuka kwa'Viswahili'na utafiti wa Kiswahili, Munyua (2002) anasema kuwa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi. Anaitumia dhana ya'Viswahili'kurejelea matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili kutokana na uhamishaji hasi kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza kama vile: Kibukusu, Kikisii, Kikikuyu, Kimeru, Kikalenjin na Kiluo. Alisisitiza kuwa athari husika hujitokeza katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kuhusu idadi ya makosa katika tamko, Munyua alishikilia kuwa iwapo makosa ni mengi, tamko husika hukanganya; hivyo kutoeleweka.

Alipendekeza kuwa tafiti zifanywe kuhusu 'Viswahili' kwa lengo la kuwaelekeza watunga mitaala ya Kiswahili kuzua mbinu mpya za ufundishaji wa Kiswahili sanifu.

Zhang (2007) alielezea kuwa si jambo la kustaajabu kuwa athari ya lugha ya kwanza inahusisha wanafunzi hata walio katika vyuo vikuu. Wanafunzi walifanya makosa walipokuwa wakijifunza Kiingereza cha kuandika na kusemwa kama lugha ya pili. Wanafunzi waliingiza miundo ya lugha ya kwanza katika Kiingereza ama lugha nyingine waliojifunza kama lugha ya pili. Zhang alijishughulisha na lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na ya Kiswahili, kumaanisha kulikuwa na haja ya kutafiti jinsi lugha hizo za kwanza zilivyo athiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili huko chuoni.

## 2.4 Dhana ya Fonolojia

Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa fonolojia ni utanzu wa isimu unaohusu jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi katika lugha mbalimbali. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa fonolojia hushugulikia jinsi sauti zinavyotumika, zinavyounganishwa na kupangwa katika lugha yoyote mahususi ili kuunda tungo zenye maana.

Mawazo haya yanawiana na maelezo ya Massamba (2004) kuwa fonolojia ni tawi la isimu linalochunguza mfumo na ruwaza za sauti za lugha mahususi ya binadamu. Basi ni muhimu kufanya utafiti wa aina hii katika lugha ya Kisomali ili kuchunguza namna sauti za lugha hii zinavyotumika na hata mpangilio wake. Aidha kwa kiasi kikubwa fonolojia hujihusisha na sheria au kanuni zinazoandamana na utoaji na utumiaji wa sauti hizo pambanuzi. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa kuna ukubalifu kwamba fonolojia ni utanzu wa isimu ambao unahusu matumizi ya sauti katika lugha mahususi.

Hii ina maana kwamba fonolojia kama tawi la isimu hujishughulisha hasa na zile sauti ambazo hutumika katika kutofautisha maana katika lugha mahususi. Aidha kwa kiasi kikubwa fonolojia hujihusisha na sheria au kanuni zinazoandamana na utoaji na utumiaji wa sauti hizo pambanuzi.

Hivyo basi tunaweza kusema kuwa fonolojia ni utanzu wa isimu ambao unachunguza sauti na matumizi yake katika lugha mahususi. Basi ni katika mtazamo huu ambapo tunaweza kusema kuwa tunaangalia fonolojia ya Kiswahili au Kisomali kwa kuchunguza sauti zake na matumizi yake katika lugha hizo.

Hii ina maana kwamba fonolojia kama tawi la isimu hujishughulisha hasa zile na sauti ambazo hutumika katika kutofautisha maana katika lugha mahususi. Aidha kwa kiasi kikubwa fonolojia hujihusisha na sheria au kanuni zinazoandamana na utoaji na sheria au kanuni zinazoandamana na utoaji na utumiaji wa sauti hizo pambanuzi. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa fonolojia ni utanzu wa isimu ambao unachunguza sauti na matumizi yake katika lugha mahususi. Basi ni katika mtazamo huu ambapo tunaweza kusema kuwa tunaangalia fonolojia ya Kiswahili au Kisomali kwa kuchunguza sauti zake na matumizi yake katika lugha hizo.

**2.5 Dhana ya Fonimu**

Njogu na Wengine (2006) wanasema kuwa fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha fonolojia kinachobadili maana ya neno. Kwa mfano mwanafunzi msemaji Kisomali anaposema neno baba na papa atakuwa akimaanisha mzazi wa kiume atasema papa badala ya baba. Tofauti katika maneno haya ni (p). Hivyo basi, kutokana na mfano huu sauti /p/ ndio inaleta utofauti wa maana katika maneno haya mawili. Kwa hivyo /p/ ni fonimu katika lugha ya Kiswahili.

Massamba na wenzake (2004) wakinukuliwa na Kanake (2013) wamefafanua kauli hii kwa kusema kuwa fonimu ni vitamkwa vinavyoweza kujenga maneno yenye maana au vinavyoweza kubadilisha maana za maneno.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza fonimu kama kipashio kidogo kabisa katika lugha, chenye kubainisha maana. Tunatumia jozi la maneno ili kuonyesha tofauti kimaana zinazoletwa na fonimu. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili maneno yafuatayo yanatofautiana katika sauti moja tu;

Saa kifaa cha kuonyesha wakati.

Taa kifaa kinachotoa mwangaza.

Tofauti za kimaana katika maneno haya mawili ni sauti /s/ na /t/ kwa hivyo sauti hizi ni fonimu kwa sababu zinasaidia kuleta tofauti kimaana kati ya maneno haya mawili.

Kwa mujibu wa Mgullu (2001) lazima mtu ajue fonimu za lugha pamoja na sifa zake na aziweke akilini mwake ndipo aweze kuzitumia ipasavyo. Zifuatazo ni sifa za fonimu.

a) Kila fonimu ina sifa zake za kifonetiki zinazoweza kuelezwa ili kuifafanua fonimu hiyo.

b) Kila fonimu ina sifa zake za kifonolojia ambazo huonyesha uamilifu wa fonimu hiyo katika lugha maalumu.

c) Wasemaji wa lugha fulani huzielewa sifa zote za fonimu za lugha yao ikiwa ni mojawapo ya sehemu ya umilisi wao wa lugha hiyo.

d) Kila fonimu hushiriki kujenga na kutofautisha maana katika neno.

e) Ukibadili fonimu katika neno bila shaka muundo au maana ya neno hilo litapotea au hata kupotoka kabisa. Kwa mfano ukichukua neno la Kiswahili “sali” na ubadilishe fonimu ya kwanza /s/ na fonimu /k/ lile neno litabadilika na kuwa “kali”, neno afisi ubadilishe fonimu /a/ na kuwa fonimu /o/ muundo utabadilika ofisi.

f) Ukiongeza fonimu katika neno lolote maana yake itapotea ama hata kubadilika. Mfano neno kuja likiongezwa fonimu /a/ litabadilika na kuwa kujaa. Neno ambalo lina maana tofauti kabisa nakuja.

g) Ukipunguza fonimu katika neno maana ya neno hilo litabadilika au kupotea.

h) Ukipangua mpangilio wa fonimu katika neno maana ya neno hilo litabadilika au kupotea.

i) Kila lugha ina fonimu zake na fonimu za lugha tofauti hazifanani kimatumizi.

Dhana ya fonimu ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu ni katika kuelewa fonimu za Kiswahili na Kisomali ambapo uhusiano wa kifonolojia utaweza kutolewa. Pia tunaelewa kuwa Kisomali na Kiswahili ziko katika makundi tofauti basi sauti zinatofautiana. Hali hii ni tatizo kubwa kwa watu wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Tunajua pia kuongeza au kupunguza fonimu katika neno hubadilisha maana katika neno. Kwa hivyo uelewaji wa fonimu utatusaidia kubadilisha iwapo athari ya Kisomali inaleta mabadiliko yoyote katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

**2.5 Irabu za Kiswahili**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu irabu za Kiswahili na wataalamu mbalimbali kutoa maoni yao. Massamba na wenzie (2004) wanaeleza irabu kama aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa pasi na kuwepo na kizuizi chochote katika mkondo hewa utokao mapafuni ukipitia katika chemba cha kinywa na chemba cha pua.

Njogu na wenzake (2006) wanaeleza irabu kama sauti ambazo katika kutolewa kwake ala za kutamkia huwa hazikaribiani kiasi cha kuweza kusababisha kukatizwa kwa hewa au kuzuiwa kwa hewa kama ilivyo katika utamkaji wa konsonanti.

Idadi ya irabu hutegemea lugha, lugha ya Kiswahili ina irabu tano.

| **Maandishi ya kawaida** | **unukuzi kifonetiki** |
|---|---|
| i | /i/ |
| e | /ɛ/ |
| a | /a/ |
| o | /ɔ/ |
| u | /u/ |

Massamba (2004) anakukubaliana na maelezo ya Mgullu (1999) kuwa lugha ya Kiswahili ina fonimu tano za irabu, ambazo ni /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ / na /u/. Katika kuainisha irabu tunaangalia vigezo viwili. Kwanza ni mahali pa kutamkia na tunapata aina tatu za irabu nazo ni irabu za mbele /i/ na /ɛ/, irabu za nyuma /u/, na /ɔ/ na irabu ya kati /a/. Pili, tunaangalia mwinuko wa ulimi. Hapo tunapata irabu za juu /i/ na /u/ na irabu ya chini /a/ na irabu za kati /ɛ/ na /ɔ/.

***Mchoro 1: Irabu za Kiswahili***




***Massamba (2004)***

## 2.6 Konsonanti za Kiswahili

Massamba na wenzake (2004) wanaeleza kuwa konsonanti ni sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni, ukipitia chemba cha kinywa na chemba cha pua kwenda nje. Ili kuelezea aina mbalimbali za konsonanti za Kiswahili tunajikita katika misingi miwili ambayo ni mahali hewa inapozuiliwa na jinsi hewa inavyozuiliwa. Misingi hii miwili ni muhimu sana katika uainishaji wa konsonanti, tunapozitamka konsonanti huwa tunahusisha sehemu saba kinywani ambazo zinaitwa ala za matamshi.

Sehemu hizi za kutamkia sauti za Kiswahili kila moja katika upekee wake ni sifa pambanuzi na zinaunda sifa bainifu kuu ya mahali hewa inapozuiliwa. Kwa kuzingatia sifa hii tunaweza kupata makundi yafuatayo ya konsonanti.

Kuna konsonanti ambazo hutamkwa kwa kubana hewa kati ya mdomo wa juu na mdomo wa chini. Kisha hewa huachiliwa kwa ghafla hii ndio sifa ya kwanza. Vitamkwa hivi ni /p/, /b/, na /m/.

Sifa ya midomo na meno hujenga kundi la pili. Kitamkwa hutamkwa kwa kugusanisha mdomo wa chini na meno ya juu. Hewa haizuiwi bali hujisukumia kati ya ala hizi na kiwango kiasi hutoka wakati wa utamkaji. Konsonanti ambazo hutamkwa kwa njia hii ni /f/ na /v/.

Sifa ya meno na ncha ya ulimi, vinapotamkwa ncha ya ulimi hugusishwa meno ya juu na kubana kidogo hewa inayosukumwa taratibu na kutoa vitamkwa /ɵ/ na /ð/.

Sifa ya ufizi. Ulimi unapogusishwa au kukaribiana na ufizi vitamkwa mbalimbali hutokea kutokana na hewa kuzuiliwa na kuachiliwa kwa ghafla. Vitamkwa vingine hutokea wakati ulimi unapigishwa kwenye ufizi. Sifa hii ndio ina vitamkwa vingi sana. Mfano wa vitamkwa ni /d/, /t/, /n/, /z/ na kadhalika.

Sifa ya kaakaa gumu. Vitamkwa hutamkwa kwa ulimi kugusa kaakaa gumu au kuufanya ukaribiane na kaakaa gumu. Konsonanti ambazo hutolewa kwa njia hii ni pamoja na /j/, /ɟ/, /ʧ/ na /ɲ/.

Kundi lingine la konsonanti huundwa kwa kutumia kaa kaa laini ambayo ni sehemu ya juu ya chemba cha kinywa iliyo nyuma ya kaakaa gumu.  Katika sehemu hii konsonanti hupatikana kwa shina la ulimi kuinuliwa na kuigusa. Vitamkwa hivi hutolewa /k/, /g/, /ɣ/ na /ɲ/.

Koromeo ni nafasi katikati ya nyuzi za sauti na koromeo. Sifa hii hutoa konsonanti moja /h/.

Msingi wa pili ni jinsi hewa inavyozuiliwa.  Kwa kuzingatia msingi huu tunapata aina saba za konsonanti za Kiswahili. Aina ya kwanza ni vipasuo. Vipasuo hupatikana wakati hewa hubanwa kabisa na baadaye kuachiliwa kwa ghafla.  Hali hii hutoa konsonanti sita katika Kiswahili nazo ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/.

| /p/ | /b/ | /t/ | /d/ |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +kip | +kip | +kip | +kip |
| +midomo | +midomo | +ufizi | +ufizi |
| -nazali | -nazali | -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna | -ghuna | +ghuna |

| /k/ | /g/ |
|---|---|
| +kons | +kons |
| +kip | +kip |
| +kaakaa laini | +kaakaa laini |
| -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna |

Vizuiwa-kwamiza ni konsonanti ambazo zinapotamkwa hewa husukumwa nje kwa nguvu, huzuiwa halafu nafasi ndogo huachwa ili hewa ipite kwa namna ya kukwamizwa. Vizuiwa-kwamiza katika Kiswahili ni viwili tu ambavyo ni /ʧ/ na / ɟ /.

| /ʧ/ | / ɟ / |
|---|---|
| +kizuiwa-kwamizwa | +kizuiwa kwamizwa |
| +kaakaa gumu | +kaakaa gumu |
| -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna |

Vikwamizwa, hali hii hutokana na kukwamizwa kwa hewa kwa kugusanisha midomo na meno kwa baadhi ya vitamkwa na vilevile kwa kugusanisha ulimi na meno, ulimi na ufizi, ulimi na kaakaa gumu na ulimi na kaa kaa laini. Vikwamizwa katika Kiswahili ni /f/, /v/ /ɵ/, /ð/, /s/, /z/, /ʃ/, /ɤ/ na /h/.

| /f/ | /v/ | /ɵ/ | /ð/, |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa |
| +midomo-meno | +midomo-meno | +meno | +meno |
| -nazali | -nazali | -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna | -ghuna | +ghuna |

| /s/ | /z/ | /ʃ/, | /ɤ/ |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa |
| +ufizi | +ufizi | +kaakaa gumu | +kaakaa laini |
| -nazali | -nazali | -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna | -ghuna | +ghuna |

Nazali ni aina nyingine. Ni aina ya konsonanti ambazo zinahusisha uzuiaji wa hewa katika sehemu mbalimbali za chemba cha kinywa na kuiruhusu ipite katika chemba cha pua. Kiswahili kina nazali nne amabazo ni /m/, /n/, /ɲ/ na /ɳ/.

| /m/ | /n/ | /ɲ/ | /ɳ/, |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +nazali | +nazali | +nazali | +nazali |
| +midomo | +midomo | +kaakaa gumu | +kaakaa laini |
| +ghuna | +ghuna | +ghuna | +ghuna |

Aina nyingine ya kundi ni kitambaza ambacho ni kimoja tu nacho ni /l/. Konsonanti hii hutamkwa kwa kutandaza ulimi kwenye ufizi na kuacha hewa kupenya pembeni mwa ulimi.

/l/

+kons
+kitambaza
+ufizi
-nazali
+ghuna

Kimadende ni konsonanti moja  ambayo inapotamkwa ncha ya ulimi hupigapiga ufizi mfululizo hii ni /r/.

/r/

+kons
+kimadende
+ufizi
+ghuna
-nazali

Kundi la mwisho kwa kuzingatia msingi wa hewa inavyozuiliwa ni kundi la kiyeyusho. Kitamkwa /j/ hutamkwa wakati midomo inakaribiana na imetandazwa na ulimi unakaribia kaakaa gumu. Kitamkwa /w/ hutamkwa wakati midomo imekaribiana imeviringwa na ulimi uko chini. Utamkaji wa konsonanti hizi hukaribiana na ule wa irabu ndiposa wakati mwingine hujulikana kama nusu-irabu. Vitamkwa hivi ni /j/ na /w/.

| /j/ | /w/ |
|---|---|
| +kons | +kons |
| +kiyeyusho | +kiyeyusho |
| +kaakaa laini | +midomo |
| -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna |

Wataalamu hawajakubaliana kuhusu idadi za konsonanti katika lugha ya Kiswahili. Kuna watafiti wanaosema kuwa kuna fonimu za konsonanti ishirini na nne, wengine ishirini na tano na hata ishirini na saba.

Mgullu (1999) anasema kuwa tatizo hili linahusu hasa mwambatano wa fonimu za nazali na fonimu zingine. Utafiti huu umetumia fonimu za konsonanti ambazo zimetumiwa na watafiti wengi ambazo ni ishirini na tano zimenukuliwa (Massamba 2004).

Massamba (2004) anaeleza kuwa utaratibu wa kupanga jedwali la konsonanti uliozoeleka ni wa kuonyesha sifa za mahali pa matamshi katika safu ya juu, kuanzia kushoto kwenda kulia: ambapo tunaanza na midomo kushoto na kuendelea hadi kufikia koromeo kulia. Sifa za jinsi ya matamshi huonyeshwa kuwa mpangilio wa kuanzia juu kushoto na kuteremka hadi chini. Utaratibu huu umetumika katika kuziainisha konsonanti za Kiswahili katika jedwali linalofuata.

**Jedwali 1: Konsonanti za Kiswahili**

| | Midomo | Midomo Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipashio | p,b | | | t, d | | k, g | |
| Vikwamiza | | f, v | ɵ, ð | s, z | ʃ | ɤ | h |
| Vipasuo-Kwamiza | | | | | ʧ, ɟ | | |
| Nazali | m | | | n | ɲ | ɳ | |
| Vitambaza | | | | l | | | |
| Vimadende | | | | r | | | |
| viyeyusho | w | | | | j | | |

***Kutoka:Massamba (2004:44)***

## 2.7 Dhana ya Mofimu

Mgullu (1999:129), anaeleza kuwa mofimu ni dhana ya kidhahania ambayo ni maana inayowakilishwa au kusitiriwa katika mofu. Matinde (2012: 101) anasema kwamba mofimu ni maana inayowakilishwa na mofu. Anaendelea kusema kuwa mofimu ni dhana ambayo ni sehemu ya umilisi kwa watumiaji wa lugha husika. Kutokana na fasili za wataalamu hawa tunaweza kufasili kuwa mofimu ni dhana dhahania ambayo ipo akilini mwa mtu, ambayo ni sehemu ya umilisi ya utumiaji wa lugha husika na inawakilishwa katika mofu.

Mgullu (1999), anasema mofu ni umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu na ambalo hudhihirika kifonolojia. Mofu ni sehemu halisi ya neno ambayo ina maana. Kwa mfano

a – na – pik – a

neno hili lina mofu nne.

a – ni mofu inayowakilisha mofimu ya nafsi ya tatu umoja.

-na – ni mofu inayowakilisha wakati uliopo.

-pik – ni mofu inayowakilisha mofimu ya mzizi wa neno.

- a – ni mofu inayowakilisha mofimu ya kiambishi tamati.

Baada ya kueleza maana ya mofimu ni muhimu tuangazie maana ya alomofu kulingana na wataalamu mbalimbali. Mgullu (1999:129) akimrejelea Richard na wenzake (1985) anasema kuwa alomofu ni umbo mojawapo kati ya maumbo kadhaa tofauti yanayowakilisha mofimu moja.

Matinde (2012:100) anadai alomofu ni maumbo mawili au zaidi yanayowakilisha mofimu moja. Anaendelea kueleza kuwa alomofu hutokea katika mazingira maalumu. Basi tunaweza kusema alomofu ni maumbo tofauti tofauti yanayowakilisha mofimu moja.

**2.8 Fonolojia ya Kisomali**

Kanake (2013) akiwanukuu (Massamba na wenzake 2004) wanasema kila lugha ya ulimwengu hujiteulia sauti mahususi, inazozitumia kutokana na sauti za ulimwengu. Kwa hivyo kiwango cha fonolojia cha lugha yoyote ile hushughulikia sauti za lugha mahususi na uchanganuzi wa sauti hizo. Kutokana na hali hii, kila lugha ina upekee kwa mujibu wa vitamkwa inavyovitumia na mifanyiko yake ya kifonolojia. Upekee huu ndio unaoleta tofauti katika mifumo ya kifonolojia ya lugha mbalimbali.

Watafiti mbalimbali wametafitia lugha ya Kisomali na hawajakubaliana idadi ya lahaja za lugha ya Kisomali. Pia (1965), anasema kuwa kuna lahaja nne kuu za lugha ya Kisomali ambazo ni lahaja ya Kiisaq, lahaja hii inazungumzwa kaskazini mwa Somalia hasa katika maeneo ya Hargeisa.

Lahaja ya Kidir inayozungumzwa magharibi mwa eneo la kaskazini hadi Ethiopia. Lahaja ya Kimudug inayozungumzwa katika eneo la Mijertinya na lahaja ya Kibenadir inayopatikana kusini mwa pwani ya Somalia hasa Mogadishu.

Lambert (1986) anasema kuwa(Enrico Cerrulli 1919) ndiye alikuwa mtu wa kwanza kuainisha lugha ya Kisomali kisayansi katika makundi manne ya kilahaja akizingatia majina ya koo.

Kundi la kwanza lilikuwa Isaaq ambalo lina lahaja ya Kiissa na Kigadabusi. Kundi la pili ni Daarood ambalo wasemaji wake wanapatikana katika maeneo ya Ogaden, Bari, Nugaal na Mudug, Ethiopia.

Kundi la tatu ni Hawiye ambalo wasemaji wake wanapatikana pwani ya Somalia hadi ufa wa Shebelle. Kundi la nne ni Sab ambalo wasemaji wake wanapatikana katika sehemu ya juu ya Juba na sehemu ya chini ya Shebelle.

Conway (2008), akimnukuu (Saeed 1999) amesema kuna lahaja tatu kuu katika lugha ya Kisomali. Lahaja ya Kikaskazini inayozungumzwa kaskazini, mashariki na sehemu za kusini mwa Somalia. Lahaja hii ilienea watu walipokuwa wakihama. Lahaja ya pili ni ya Kibenadir inayotumiwa kusini mwa pwani ya Somalia hasa Mogadishu. Lahaja ya tatu ni Kimay inazungumzwa kusini mwa pwani ya Somalia. Lahaja ya Kikaskazini inatumiwa kama Lingua Franka katika mawasiliano na koo zingine za Kisomali.

Mohamed (2013) anasema kuwa lugha ya Kisomali imengawanya lahaja katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lahaja za Kimaxatiri ambazo hutumiwa katika shughuli rasmi, zinazungumzwa kaskazini, magharibi na kusini mwa Somalia, pia zinajulikana kama Lingua Franka ya Somalia. Kundi la pili lahaja za Kibenadir zinazozungumzwa pwani ya Somalia na Mogadishu. Kundi la tatu ni lahaja za Kimay zinayozungumzwa kusini magharibi mwa Somalia na zimesambaa hadi mpaka wa Ethiopia.

Kevogo na wenzake (2015) wakimnukuu (Lambert 1986) wanasema alianisha lahaja za lugha ya Kisomali katika makundi matano. Kundi la kwanza ni Kisomali cha kaskazini ambalo lina lahaja ya Kaskazini, lahaja ya Kidaarood, lahaja ya Kijuba cha chini. Kundi la pili ni Benadir, ambalo lina lahaja ya Kiabgaal, Lahaja ya Kiajuraan, lahaja ya Kiaaljacal, lahaja ya Kixaman na lahaja ya Kibimaal. Kundi la tatu ni Ashraaf, ambalo lina lahaja ya Kishangaani na lahaja ya Kishebelle ya chini.

Kundi la nne ni Maay na la tano ni Digil ambalo lina lahaja ya Kitunni, lahaja ya Kidabarre, lahaja ya Kigarre na lahaja ya Kijiiddu. Lahaja ya Kidaarood ndiyo inatumika sehemu za kaskazini mashariki nchini Kenya (Kevogo na wenzake 2015).

Utafiti huu ulitumia lahaja ambazo zimebainishwa na Lamberti (1986) kwa sababu zilikuwa zimefafanuliwa kwa kina. Kevogo na wenzake (2015) walitumia lahaja hizo na kuweza kubaini kuwa lugha ya Kisomali nchini Kenya huwakilishwa na lahaja ya Kidaarood. Lahaja ambayo ilitumiwa na wao kubaini mtazamo wa wasemaji wa lugha ya Kisomali katika utumiaji wa lugha ya Kiswahili.

**2.9 Fonimu za Irabu za Kisomali**

Mohamed (2013) anasema kuwa lugha ya Kisomali ina vokali tano. Vokali zote zinaweza kuwekwa katika makundi mawili: vokali ndefu na vokali fupi kulingana na matamshi.

**Jedwali 2: Fonimu za konsonanti za Lugha ya Kisomali**

| **Vokali fupi** | | | **Vokali ndefu** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| <a> | <yár> | taarifa | <aa> | <náa> | titi |
| <ɛ> | <sɛxó> | lala | <ɛɛ> | <gɛɛd> | mti |
| <i> | <bír> | chuma | <ii> | <wíil> | mvulana |
| <ɔ> | <cɔl> | adui | <ɔɔ> | <rɔɔb> | mvua |
| <u> | <kún> | elfu | <uu> | <búuk> | kitabu |

***Kutoka: Mohamed (2013)***

Irabu za mbele ni/ɛ/na /ì/ kwa sababu zinatamkiwa sehemu ya mbele ya ulimi. /a/ ni irabu ya mbele ambayo hutamkiwa katika ncha ya ulimi. /ɔ/ na /u/ ni irabu za nyuma kwa kuwa zinatamkiwa katika sehemu ya nyuma ya ulimi.

## 2.10 Fonimu za konsonanti za Kisomali

Mohamed (2013) akimnukuu (Koffi, 2012) anasema kuwa lugha ya Kisomali ina fonimu za kosonanti ishirini na mbili.

**Jedwali 3: Fonimu za konsonanti za lugha ya Kisomali**

| | **Midomo** | **Midomo Meno** | **Meno** | **Ufizi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **Koromea** | **Glota** | **Uvuli** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Vipasuo tulivu** | | | | t | | k | | ʔ | |
| **Vipasuo lipuzi** | b | | ð | ɗ | | g | | | G |
| **Vikwamizwa tulivu** | | f | | s | ʃ | | ħ | | χ |
| **Vikwamizo lipuzi** | | | | | | | ʕ | | |
| **Vipasuo-Kwamizwa** | | | | | ʧ | | | | |
| **Nazali** | m | | | n | | | | | |
| **Vitambaza** | | | | | | l | | | |
| **Vimadende** | | | | r | | | | | |
| **Nusu-irabu** | w | | | | | j | | | |

***Kutoka: Koffi (2012)***

Namna ambavyo konsonanti hizi zinavyojitokeza katika matamshi sivyo zote zinavyowakilishwa katika othografia. Jedwali lifuatalo linaonyesha konsonanti za Kisomali na namna zinavyowakilishwa katika othografia.

**Jedwali 4: Unukuzi wa fonimu za kosonanti za Kisomali kiothografia**

| Herufi | Mnukuu | Neno la Kisomali | Katika Kiswahili |
|---|---|---|---|
| B | /b/ | [buːg] | Kitabu |
| C | /ʕ/ | [ʕunta] | Chakula |
| D | /ɗ/ | [ɗuːl] | Ardhi |
| F | /f/ | [far] | kidole |
| G | /g/ | [gɛbir] | msichana |
| H | /h/ | [hɔːyɔ] | mama |
| J | /j/ | [jƐƐg] | Jagi |
| K | /k/ | [kaːlƐ] | Njoo |
| L | /l/ | [libaːħ] | simba |
| M | /m/ | [magaʕ] | jina |
| Q | /G/ | [Gubɛj] | Chupa |
| R | /r/ | [rɔːb] | Mvua |
| S | /s/ | [saʕ] | ngʾombe |
| T | /t/ | [taːrɔ] | mawaidha |
| W | /w/ | [warɗijƐ] | mlinzi |
| X | /ħ/ | [ħarifa] | mwerevu |
| Y | /j/ | [biːja] | Maji |
| SH | /ʃ/ | [ʃaGaɗ] | Kazi |
| DH | /ð/ | [ðɛːr] | Nguo |

***Kutoka: Mohamed (2013)***

## 2.11 Dhana ya Mofolojia

Besha (2007:49) anasema mofolojia ni taaluma inayojishughulisha na kuchambua muundo wa maneno katika lugha. Massamba na wenzake (2009:32) wanasema kuwa mofolojia ni kiwango

cha sarufi kinachojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha, yaani jinsi ambavyo maneno ya lugha yoyote iwayo ile yanaundwa. Wataalamu hawa wawili wanaonekana kuingiliana katika kuonyesha namna taaluma ya mofolojia inavyojihusisha na muundo wa maneno katika lugha. Rubanza (1996:1) anaonekana kuungana nao kwa kusema kwamba mofolojia ni taaluma inayojishughulisha na vipashio vya lugha na mpangilio wake katika uundaji wa maneno. Mtaalamu huyu anaongeza kwamba mofolojia huzingatia namna vipashio vinavyotumika katika kupangilia mfumo wa muundo wa maneno katika lugha. Kipashio cha msingi katika kiwango hiki cha isimu ni mofimu.

John Habwe na Peter Karanja (2004) wanasema ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa maneno. Kutokana na fasili za wataalamu hawa tunaweza kueleza kuwa; mofolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa maumbo ya maneno katika lugha mahususi.

**2.12 Dhana ya Mofofonolojia**

Neno mofofonolojia limeundwa na maneno mawili mofolojia na fonolojia. Maneno haya huwakilisha viwango tofauti katika usomaji wa isimu. Fonolojia ni utanzu wa isimu ambao unahusu matumizi ya sauti katika lugha mahususi. Mofolojia ni utanzu wa isimu unaojishughulisha na uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa maumbo ya maneno katika lugha mahususi.

Maneno haya mawili yanahusiana kwa kuwa kanuni za kifonolojia zinaweza kutumiwa kuelezea maumbo ya kimofolojia, kanuni hizi si za kueleza maumbo tu bali pia huweza kubadili umbo la neno; yaani umbo la ndani na umbo la nje. Kwa hivyo maneno haya yakiunganishwa yatakuwa mofofonolojia.

Massamba (2010: 82) akimrejelea Martnet (1965) anafafanua kwamba, istilahi ya mofofonolojia ilipendekezwa mara ya kwanza na Trubetzkoy (1929). Trubetzkoy alitumia istilahi hii kwa maana ya tawi la isimu linaloshugulikia matumizi ya mofolojia katika kueleza

baadhi ya tofauti za kifonolojia ambazo zisingewezekana kuelezewa kwa kutumia data za kifonolojia au kifonetiki peke yake.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Kitangulizi

Utaratibu wautafiti, jumuia na uteuzi wa sampuli, eneo la utafiti, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data zimeangaziwa katika sura hii.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umechunguza jinsi athari ya lugha ya Kisomali na hasa lahaja ya Kidaarood ambayo wasemaji ndio wanaopatikana katika eneo la Garissa Township, jinsi ilivyotatiza ufunzaji wa lugha ya Kiswahili. Tulishughulikia vokali, konsonanti na uundaji wa maneno kwa hivyo tulijishughulisha na kipengele cha kifonolojia na mofolojia ambavyo vikiunganishwa huwa kimofofonolojia, kwa kuwa umilisi wa sauti za lugha yoyote ni njia mwafaka ya kuelewa fonolojia ya lugha husika. Tuliwashirikisha wanafunzi watano wa kidato cha tatu, kutoka shule sita za kutwa katika kaunti–ndogo ya Garissa –Township ambazo zilikuwa zimeteuliwa. Idadi ya wanafunzi walioshirikishwa ni thelathini. Hii ni kwa sababu wanafunzi waliohudhuria masomo shule hizi ni wazawa wa eneo hili. Walio katika kidato cha kwanza na pili hawajapata umilisi wa kiwango fulani cha lugha ya Kiswahili, ilhali walio katika kidato cha tatu walikisiwa kuwa wamepata umilisi wa kiwango fulani cha lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa wanajitayarishia mitihani ya kitaifa na kuwashirikisha katika utafiti huu tungekuwa tunawasumbua.

### 3.3 Utaratibu wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya utaratibu wa nyanjani ambao ulihusisha utumiaji wa hojaji kwa lengo la kuhakikisha walikuwa wasemaji asilia wa lugha ya Kisomali jambo ambalo lilimuwezesha mtafiti kupata data bora. Utaratibu wa nyanjani ulitumika ili kupata maandishi ya kina kwa lengo la kuwapata wanafunzi ambao wanafanya makosa ya kimofofonolojia.

Mtafiti alitumia insha (Tazama Kiambatanisho cha nne). Wanafunzi waliandika insha yenye mada ***SIKU AMBAYO SITAISAHAU*** wakizingatia mada hiyo waliyopewa na mtafiti, hawakupimiwa wakati lakini walitakiwa kuandika insha zenye urefu wa maneno mia tatu na sabini na tano au kurasa mbili. Mtafiti alipitia insha zote ambazo alikusanya kwa makini, huku akitambua makosa ya kimofofonolojia ambayo wanafunzi wamefanya.

Kishawalisimulia hadithi wazipendazo, (Tazama Kiambatanisho cha tatu). Kwa kufanya hivi wanafunzi walikuwa na nafasi ya kuchagua hadithi ambazo walizielewa kwa urahisi. Mtafiti alikuwa akirekodi kila mwanafunzi alipoongea.

### 3.4 Jumuiya na Uteuzi wa Sampuli

Gay (1982 akinukuliwa na Ngowa, 2015) alisema kuwa mtafiti huwa anachagua sampuli kwa sababu huwa kuna vipingamizi fulani ambavyo havimruhusu kutafiti vipengele vyote. Utafiti huu ulilenga shule za upili za umma ambazo ni nane katika kaunti ndogo ya Garissa Township. Shule hizi zilijumuishwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lile limepata gredi ya D na kwenda chini, kundi la pili ni lile limepata gredi ya D+ na C- na la mwisho na la tatu ni lile limepata gredi ya C na kwenda juu. Kwa kuzingatia matokeo ya somo la Kiswahili katika Mtihani wa Kuhitimu wa Kitaifa wa Sekondari mwaka wa elfu mbili kumi na sita kwa sababu mtihani wa mwaka huu haukuwa na visa vingi vya undanganyifu basi ulionyesha umilisi wa mwanafunzi.

Pili, ndio mtihani ambao ulifanywa na wanafunzi wote katika kaunti-ndogo ya Garissa Township. Sampuli makundi ilitumika kuteua shule za upili za ummakatika kaunti ndogo ya Garissa Township.

Tumetumia mbinu ya uteuzi wa kimaksudi kuteua shule mbili katika kila kundi. Na pia kuteua wanafunzi wa kidato cha tatu katika kila shule ambayo iliteuliwa. Kisha njia ya sampuli nasibu ilitumiwa kuteua wanafunzi watanokutoka kidato cha tatu ili gharama ya utafiti isiwe ya juu sana. Idadi ya wanafunzi ilikuwa wanafunzi thelathini, wasichana kumi na watano na wavulana kumi na tano sababu ya kuwa na idadi hiyo ya watafitiwa ni kuhakikisha gharama ya utafiti iwe ya chini.

Hii ilikuwa sampuli wakilishi ya kundi lengwa ambalo ni shule zote za upili za umma katika kaunti ndogo ya Garissa Township. Wanafunzi wa kidato cha tatu walichanguliwa kwa kuwa inakisiwa wanaelewa sarufi ya lugha ya Kiswahili kufikia hapo. Wanaweza kujieleza vizuri bila ya kuogopa ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha pili na cha kwanza ilhali wanafunzi wa kidato cha nne hawana mda wa kushiriki katika mchakato kama huu kwa kuwa wanajitayarishia kwa mtihani wa kitaifa.

### 3.5 Vifaa vya Kukusanyia Data

Kwa kawaida utafiti wowote lazima uwe na vifaa vya kukusanyia data. Utafiti huu ulitumia vifaa vifuatavyo vya ukusanyaji wa data.

#### 3.5.1 Insha

Kifaa cha kwanza ni insha. Baada ya kuteuwa wanafunzi watakaoshirikishwa, mtafiti aliwapatia wanafunzi mada waliyozingatia wakiandika insha. Wanafunzi hawakupimiwa muda lakini walitakiwa kuandika insha yenye urefu wa maneno mia tatu sabini na tano. Walipomaliza kuandika mtafiti alikusanya insha hizo.

Baadaye mtafti alikuwa na mda wake wakusoma insha moja baada ya nyingine huku akinakili makosa ya kimofofonolojia yaliyojitokeza. Mtafiti alikuwa akiongozwa na maswali ya utafiti. Pia akizingatia hatua ambazo zinapatikana katika nadharia ya uchanganuzi makosa. Kifaa cha insha kilitumiwa kwa kuwa kinadhihirisha umilisi katika lugha fulani. Pia njia mojawapo ya kuonyesha umilisi ni kuandika.

### 3.5.2 Hadithi

Wanafunzi walipomaliza kuandika insha, walitakiwa kusimulia hadithi mmoja baada ya mwingine. Mwanafunzi alizingatia mada ambayo alitaka, hakuna mada iliyokuwa imeteuliwa. Kila mwanafunzi alipewa muda wa dakika kumi na tano kusimulia hadithi. Mtafiti alikuwa anarekodi mwanafunzi akihadithia. Baada ya kutoka nyanjani mtafiti alisikiliza kanda yake kwa makini ili kubaini makosa ya kimofofonolojia yaliyojitokeza. Sawa na kifaa cha insha, kifaa cha hadithi iteuliwa kwa kuwa kwa kuzungumza msemaji atadhihirisha umilisi katika lugha fulani.

## 3.6 Ukusanyaji wa Data

Tulizuru shule ambazo tulilenga kupata data na kufanya uhusiano mwema kabla ya siku ya kukusanya data, tuliomba ruhusa kutoka kwa mwalimu mkuu baada ya kujitambulisha rasmi. Kwa kutumia njia ya sampuli nasibu tuliteua wanafunzi watano ambao tuliwashirikisha katika utafiti kutoka kila shule, kati ya zile tulikuwa tumeteuwa. Wanafunzi walihitajika kuandika insha na wasimulie hadithi kwa kuzingatia mada waliyotaka ili kubainisha athari ya Kisomali wanafunzi wanapozungumza Kiswahili kama L2. Kwa kufanya hivyo mtafiti alipata data ya makosa ya kimofofonolojia ambayo ilimsaidia mtafiti kutambua chanzo cha makosa hayo na kanuni ambazo zinadhibiti hayo makosa.

## 3.7 Uchanganuzi wa Data

Data ya utafiti ilichanganuliwa kupitia njia ya maelezo. Athari za irabu zitaangaziwa kwanza kisha athari za konsonanti zifuate, athari zilishughulikiwa moja baada ya nyingine kwa kina. Katika kuchanganua data tulikuwa tukiongozwa na hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Makosa lakini hatua mbili za mwisho hazikuzingatiwa katika utafiti ili usiwe mpana na kuchukua muda mrefu. Mtafiti alikusanya sampuli za data alizopata nyanjani ambazo ni insha zilizoandikwa na kanda zilizorekodiwa. Pili, alitambua makosa yaliofanywa na wanafunzi ni ya aina gani. Hatua ya tatu mtafiti aliainisha makosa na kushughulikia makosa ya kimofofonolojia ambayo yalilegwa na utafiti huu. Makosa yalihesabiwa ya kila kategoria.

Baada ya hilo vipengele vyenye matatizo vilionyeshwa. Lililofuata ni mtafiti kuelezea chanzo cha makosa haya.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu lazima tuzingatie maadili kwa watafitiwa ili kutoa taarifa za kweli bila ya woga. Kwa mujibu wa Sture (2010) mkabala wa maadili ni mojawapo ya maswala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Pia Adam (2008) ametaja maadili ya utafiti ni haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatatoa siri za watafitiwa.

Anafafanua kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikisha usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakavyopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Mtafiti alitumia kibali alichopewa na chuo na kuomba vibali kutoka kwa serikali ya kaunti ili kujitambulisha na kuwahakikishia usalama watoao taarifa zao. Mtafiti alifuata mchakato wote wa uongozi katika maeneo ya kukusanya data.

Kwanza alizuru ofisi ya mkuu wa elimu katika kaunti ya Garissa na kuazima makala ya matokeo ya mtihani wa kitaifa ambayo yalihifadhiwa kwa siri sana, hii ni baada ya kujitambulisha. Mtafiti alikuwa ametayarisha fomu za kuomba idhini kutoka kwa watoto. Walimu waliwaruhusu wanafunzi kushiriki katika shughuli hii kwa kuwa ndio walezi wao shuleni. Siku ya kukusanya data tulizuru ofisi ya mwalimu mkuu kujitambulisha rasmi.

Wakati wa kuwa na uhusiano mwema na washiriki, mtafiti aliwahakikishia kuwa data waliyopatiana itatumiwa katika utafiti huu na utambulishaji wao utahifadhiwa na utakuwa wa siri. Mtafiti aliwashukuru washiriki kwa kufanikisha utafiti.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO

## 4.1 Kitangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia pamoja na kueleza sababu zilizowapelekea wanafunzi kufanya makosa haya. Makosa yameorodheshwa na kupangwa katika makundi tofauti na sehemu ambamo yanapatikana. Makosa haya yameainishwa baada ya insha za watafitiwa kusahihishwa na kanda zilizorekodiwa kuchanganuliwa ili kubaini makosa ya kimofofonolojia.

Makosa haya ni yale yanayodhihirika miongoni mwa wazungumzaji wa Kisomali wanapojifunza Kiswahili. Makosa mengine yaliyojitokeza na ambayo hayakuhusu tatizo la utafiti yalipuuzwa. Makosa haya ni kama vile uakifishaji, sintaksia, na kadhalika. Hii ni kwa sababu upeo wa tatizo la utafiti huu ni uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia na si makosa mengine yanayotokana na kategoria zingine.

Baada ya kuyaainisha makosa na kuyaweka katika kategoria mbali mbali, nilitoa visababishi vya makosa hayo. Kila lugha huwa na mfumo wake maalumu unaofaa kufuatwa katika uundaji wa maneno. Ikiwa mfumo huo hautafuatwa basi lugha hiyo itakuwa imetumiwa visivyo. Aghalabu wasemaji wa Kisomali huhamisha mifumo ya lugha yao wanapotumia Kiswahili na kupata maumbo yasiyo sahihi. Hii husababisha utata wa maana na wakati mwingine hata maana iliyokusudiwa kupotea kabisa.

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na ulishirikisha shule za kutwa za umma sita katika kaunti ndogo ya Garissa-Township. Wanafunzi walioshirikishwa ni wa kidato cha tatu.

Walishiriki katika uandishi wa insha na kuhadithia hadithi. Wanafunzi watano walichaguliwa kutoka kila shule, kwa hivyo kwa jumla wanafunzi walioshiriki ni thelathini.

Kwanza walijaza fomu ili kuhakikisha kuwa watakaohusishwa ni wale tu wanaosema lugha ya Kisomali kama lugha yao ya kwanza.

Wanafunzi waliandika insha juu ya mada ***SIKU AMBAYO SITAISAHAU*** wanafunzi walipewa muda wa kutosha wa kuandika insha bila kupimiwa muda. Hata hivyo walitakiwa waandike insha isiyopungua maneno mia tatu sabini na tano au kurasa mbili za karatasi walizopewa. Ilitarajiwa kwamba kupitia uandishi wa insha wanafunzi hawa watadhihirisha athari za Kisomali katika Kiswahili na kuhadithia kisa chochote katika lugha ya Kiswahili huku mtafiti akinakili. Mtafiti alisaidiana na walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili katika shule husika.

Katika uchanganuzi wa makosa haya tuliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Corder. Kwa mujibu wa Corder 1974, mtafiti hufuata hatua zifuatazo katika uchanganuzi makosa.

1. Kukusanya sampuli ya wanaojifunza lugha.
2. Kutambua makosa.
3. Kueleza makosa kwa kuyaweka katika makundi.
4. Kuhesabu makosa.
5. Kutambua vipengele vyenye matatizo.
6. Kufafanua visababishi vya makosa hayo.

**4.2 Kukusanya Sampuli ya wanaojifunza Lugha**

Utafiti huu ulilenga shule zote za upili za umma katika kaunti ndogo ya Garissa Township. Shule hizi zilijumuishwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lile limepata gredi ya D na kwenda chini, kundi la pili ni lile limepata gredi ya C- na D+ na la mwisho na la tatu ni lile limepata gredi ya C na kwenda juu. Hii ilisaidia katoka kuweka shule katika makundi ili kupata data. Gredi hizi zilipatikana kutokana na matokeo ya somo la Kiswahili ya mtihani wa kitaifa wa kuhitimu wa sekondari mwaka wa elfu mbili na kumi na sita. Sampuli makundi ilitumika kuteua shule za upili za umma katika kaunti ndogo ya Garissa Township. Njia ya uteuzi wa kimaksudi ilitumiwa kuteua shule mbili kila kundi. Na pia kuteua wanafunzi wa kidato cha tatu katika kila shule ambayo iliteuliwa, kisha njia ya sampuli nasibu ilitumiwa kuteua wanafunzi watano kutoka kidato cha tatu. Idadi ya wanafunzi ilikuwa wanafunzi thelathini,

idadi hii ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuishughulikia ipasavyo, kwa hivyo washiriki wote walikuwa thelathini. Hii ilikuwa sampuli wakilishaji la kundi lengwa ambalo ni shule zote za upili za umma katika kaunti ndogo ya Garissa Township.

**4.3 Kutambua Makosa**

Baada ya kutoka nyanjani na sampuli za data, mtafiti alichanganua na kuipanga huku akiongozwa na nadharia ya Corder. Mtafiti alikusanya sampuli za data alizopata nyanjani ambazo ni insha zilizoandikwa na kanda zilizorekodiwa. Hili lilimpelekea kutambua makosa yaliyofanywa na wanafunzi ambayo yalikuwa ya kisemantiki, kisintaksia, kihijai, kimofolojia na kifonolojia. Kisha mtafiti aliainisha na kushughulikia makosa ya kimofofonolojia ambayo yalilengwa na utafiti huu. Kategoria zingine za makosa hazikushughulikiwa .

**4.4 Kueleza Makosa kwa kuyaweka katika Makundi**

Makosa ya kimofofonolojia yaliwekwa katika makundi matatu ambayo ni makosa ya udondoshaji, makosa ya uchopekaji na makosa ya ubadilishaji. Makundi haya hayakuwasilisha hapa kwa kuwa hayakujaliwa kwa kina. Kwa kushughulikia haya kwa kina kungepotosha utafiti kwa kuwa hili si miongoni mwa maswali ya utafiti.

**4.5 Kuhesabu Makosa.**

Idadi ya makosa yaliyopatikana kuwa yamefanywa yalikuwa ya juu sana tukijumuisha pamoja na makosa kutoka katika kategoria zingine kama vile sintaksia, semantiki, na kadhalika. Makosa ya kategoria ya kimofofonolojia ndiyo yalishughulikiwa, makosa ya kategoria zingine hayakushughulikiwa ili utafiti usipotoke.

Hatua ya kwanza kukusanya sampuli ya wanaojifunza lugha, hatua ya pili kutambua makosa, hatua ya tatu kueleza makosa ya kuyaweka katika makundi na hatua ya nne kuhesabu makosa hazikujadiliwa kwa kina lakini zilisaidia kutoa maelezo zaidi katika hatua ya tano. Hatua ya tano kutambua vipengele vyenye matatizo ndivyo vilifafanuliwa zaidi, tukizingatia makosa ya kimofofonolojia ambayo ndio utafiti wenyewe.

Makosa yote yaliyofanywa yalikuwa mia moja ishirini na nane. Wasichana walifanya makosa themanini, hii ilikuwa asilimia sitini na tatu ya makosa yote. Hili lilitokana na kuwa wasichana hawakuwa na muda wa kutangamana na vijana wengine katika shughuli nyingine. Wasichana walikuwa na athari zaidi katika /p/ /z/ na /v/ walijipata wakitumia sauti ambazo zinakaribiana na hizi. Sauti /p/ /z/ na /v/ hazipatikani katika konsonanti za lugha ya Kisomali. Wavulana walifanya makosa arobaini na nane, ambayo ilikuwa asilimia thelathini na saba ya makosa yote. Wavulana ndio waliokuwa na idadi ya chini ya makosa kwa kuwa walishirikiana na vijana wengine katika shughuli za nje ya nyumba.

Sawasawa na wasichana walikuwa na athari ya sauti /p/, /z/ na /v/ zaidi walipokuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili.

Hatua ya sita, kufafanua visababishi vya makosa hayo haikushuhgulikiwa kabisa kwa kuwa hili halikuwa katika swala la utafiti na kufanya hivyo utafiti ungekuwa mrefu na kuchukua muda na gharama zaidi.

### 4.6 Mageuzi ya vokali.

Vokali za lugha ya Kiswahili zimepitia mageuzi katika mifanyiko mbalimbali ya kimofofonolojia ambayo yamedhihirisha makosa yanayotokea pale ambapo zinatamkwa na msemaji wa lugha ya Kisomali. Michakato ya kimofofonolojia ambayo imeweza kubainika ni uchopekaji wa vokali, udondoshaji wa vokali na ubadala wa vokali.

Hili linadhihirishwa kwa kina kama ifuatavyo :

#### 4.6.1 Udondoshaji wa vokali

Mchakato wa udondoshaji katika utafiti huu umetokea pale ambapo vokali inapatikana kati ya konsonanti mbili au mwishoni mwa neno baada ya konsonanti. Vokali mbalimbali zimedondoshwa kama ifuatavyo:

#### 4.6.1.1 Udondoshaji wa /i/

Vokali **/i/** imedondoshwa katika mazingira ya katikati ya konsonanti mbili na mwishoni mwa neno baada ya konsonanti; Mifano ifuatayo inadhihirisha mchakato huu.

**Jedwali 4: Udondoshaji wa /i/**

| Neno sahihi | Neno lenye athari. |
|---|---|
| Asubuhi | Asubuh |
| Furahi | Furah |
| Kijani | Kijan |
| Mahakamani | Mahakaman |
| Wageni | Wagen |
| Ishirini | Ishirin |
| Lakini | Lakin |

Katika mfanyiko huu, imeonekana kwamba vokali /i/ imedondoshwa kutokana na kupatikana katikati ya konsonanti na kutoka mwishoni mwa neno ikifuata konsonanti. Hii ni kusema kuwa vokali /i/ imekuwa kapa. Kutokana na mfanyiko huu, kanuni ya kimofofonolojia inaweza kuwa.

Kanuni: /i/ ⟶ /Ø/ / +K

#### 4.6.1.2 Udondoshaji wa /a/.

Irabu /a/ inadondoshwa pale ambapo inatokea mwisho wa neno na inafuatwa na konsonanti na ikitokea katika mifano inayodhihirisha mfanyiko huu ni:

**Jedwali 5: Udondoshaji wa /a/**

| Neno sahihi | Neno lenye athari |
|---|---|
| Alienda | Aliend |
| Waliletwa | Waliletw |
| Napenda | Napend |
| Matangazo | Mtangazo |
| Baadaye | Badaye |

Kanuni: /a/ ⟶ /Ø/ ⁄ +K

Ni dhahiri katika kanuni hii kuwa vokali /a/ inaachwa wakati inapopatikana mwisho mwa neno huku ikifuatwa na konsonanti. Hili linatokea kwa sababu lugha ya Kiswahili na lugha ya Kisomali zina mfumo tofauti wa silabi, Kiswahili kinatumia silabi wazi ilhali Kisomali kinatumia silabi funge. Basi wasemaji wa lugha hii ya Kisomali wanahamisha mfumo huo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili ambao ni makosa.

### 4.6.1.3 Udondoshaji wa irabu /ɛ/.

Irabu /ɛ/ imedondoshwa pale ambapo imetokea ikifuatana na irabu nyingine /ɛ/.

Mifano inayodhihirisha mchakato huu ni:

**Jedwali 6: Udondoshaji wa irabu /ɛ/.**

| Sahihi | Neno lenye athari |
|---|---|
| Ameendesha | Amendesha |
| Nimeenda | Nimenda |
| Tumeeleza | Tumeleza |
| Ameelimika | Amelimika |

Kanuni: /ɛ/ ⟶ /Ø / ⁄ I-K

Katika sheria iliopo hapa juu irabu /ɛ/ inapopatikana katika mazingira ya katikati mwa neno, kati ya irabu /ɛ/ na konsonanti yoyote ile hudondoshwa. Hili linafanyika kwa kuwa katika lugha ya Kisomali hakuna mfuatano wa vokali mbili ilhali katika lugha ya Kiswahili kuna mfuatano wa aina hiyo.

#### 4.6.1.4 Udondoshaji wa irabu /u/

Vokali /u/ inadondoshwa pale ambapo inatokea katikati mwa kosonanti au mwishoni mwa neno na inafuata konsonanti. Mifano inayoafiki hili ni:

**Jedwali 7: Udondoshaji wa irabu /u/.**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Sanduku | sanduk |
| Mbegu | mbeg |
| Kakangu | Kakang |
| Langu | lang |

Kanuni : /u/ ⟶ /Ø/ / +K

Katika kanuni hii hapa juu ni dhahiri kwamba irabu /u/ inakuwa kapa pale ambapo inapatikana mwishoni mwa neno ikifuatwa na konsonanti ambayo ni kipasuo, kinachotamkiwa katika kaakaa laini. Lugha ya Kisomali huwa na silabi funge na mfumo huu wa silabi ndio unatumiwa na wasemaji hawa wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

### 4.6.2 Ubadala wa Vokali

Vokali zinazopatikana katika maneno ya Kiswahili zimeonekana zikipitia mageuzi ili kudhihirisha athari ya Kisomali katika lugha ya Kiswahili. Mchakato huu umehusisha mabadiliko ya vokali mbalimbali kama ifuatavyo:

**4.6.2.1 Ubadala wa irabu /i/ > /ɛ/.**

Irabu /ɛ/ imeonekana kutumiwa badala ya irabu /i/.

Ufuatao ni mchakato unaodhihirisha ubadala wa vokali hizi. Mifano ya maneno yaliyosawiri mchakato huu wa ubadala wa vokali ni kama ifuatayo;

**Jedwali 8: Ubadala wa irabu /i/ > /ɛ/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Tiliposhikwa | Tuliposhekwa |
| Hivyo | Hevyo |
| Tukaachiliwa | Tukaacheliwa |
| Mwisho | Mwesho |
| Kuwika | Kuweka |
| Alikimbia | Alikembia |
| Kortini | Korteni |
| Polisi | Polesi |
| Mingi | Mengi |

Kanuni : /i/ ⟶ /ɛ/ / K-K

Sheria iliyopo hapa juu inadhihirisha kuwa vokali /i/ inapotokea katikati mwa konsonanti mbili katika neno la kiswahili, inabadilika na kuwa vokali /ɛ/ kwa hivyo vokali hii ndio hutumiwa badala ya vokali /i/.

**4.6.2.2 Ubadala wa irabu /a/ >/ɔ/.**

Wasemaji wa Kisomali walitumia irabu /ɔ/ pale ambapo walitakiwa kutumia /a/. Mifano ya maneno yaliyosawiri mabadiliko haya ni kama ifuatayo;

**Jedwali 9: Ubadala wa irabu /a/ > /ɔ/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Ng'ambo | Ng'ombo |
| Gari | Gori |
| Mayowe | Moyowe |
| Makofi | Mokofi |
| Kambo | Kombo |
| Karo | Koro |

Kanuni : /a/ ⟶ /ɔ/ / K-K

Kanuni tuliotaja hapo juu inaafiki kuwa vokali /ɔ/ inatumika pale ambapo /a/ inajipata katikati ya konsonanti mbili wakati msemaji wa lugha ya Kisomali anatumia lugha ya Kiswahili.

**4.6.2.3 Ubadala wa irabu /u/ > /ɔ/.**

Vokali /u/ inayopatikana katika lugha ya Kiswahili imepitia mabadiliko na kuchukua umbo la vokali /ɔ/ ambayo inayotumika katika lugha ya Kisomali.

Mifano ya nomino zilizosawiri mabadiliko haya ni kama zifuatazo;

**Jedwali 10: Ubadala wa irabu /u/ > /ɔ/.**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Tumbo | Tombo |
| Arusi | Arose |
| Nitakununulia | Nitakonunulia |
| Rudi | Rodi |
| Rungu | Rongu |
| Shule | Shole |

Kanuni : /u/ ⟶ /ɔ/ / K-K

Sheria iliotaja hapa juu inaonyesha kuwa vokali /ɔ/ inatumika badala /u/ wakati /u/ inapotokea katikati mwa konsonanti mbili. Jambo hili linalotokea linaonyesha kuudhoofika kwa kwa sauti. Kwani /u/ ambayo huwa vokali ya juu inashuka na kuwa /ɔ/ ambayo ni vokali ya kati.

**4.6.2.4 Ubadala wa /ɛ/ > /i/.**

Vilevile vokali /ɛ/ ya lugha ya Kiswahili ilionekana kupitia mageuzi na kuwa /i/ ili kudhihirisha makosa haya ya kimofofonolojia kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

**Jedwali 11: Ubadala wa /ɛ/ > /i/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Kesho | Kisho |
| Tumebarikiwa | Tumibarikiwa |
| Walisema | Walisima |

Kanuni : /ɛ/ ⟶ /i/ / K-K

Katika sheria tuliotaja hapa juu ni dhahiri kuwa vokali /ɛ/ inapotokea katikati mwa konsonanti mbili inabadilika na kuwa vokali /i/. Hili linadhihirisha kuimarika kwa sauti kwa sababu vokali /ɛ/ ni vokali ya chini na inabadilika na kuwa /i/ ambayo ni ya juu.

**4.6.2.5 Ubadala wa vokali /ɛ/ > /a/**

Irabu /ɛ/ ya lugha ya Kiswahili inapitia mfanyiko na kuwa /a/ katika lugha ya Kisomali. Basi makosa ya kimofofonolojia hutokea. Mifano ifuatayo inaafiki haya;

**Jedwali 12: Ubadala wa vokali /ɛ/ > /a/.**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Upande | Upanda |
| Ambaye | Ambaya |
| Naye | Naya |
| Pale | Pala |

Kanuni : /ɛ/ ⟶ /a/ / **+k**

Katika sheria tuliotaja vokali /ɛ/ inabadilika na kuwa /a/ pale ambapo inatokea mwishoni mwa neno na inafuatwa na konsonanti. Huku ni kuimarika kwa sauti kwani /ɛ/ ni sauti ya chini na inakuwa /a/ ambayo ni ya kati.

**4.6.2.7 Ubadala wa /ɔ/ > /ɛ/.**

Irabu /ɔ/ya Kiswahili inapitia mchakato na kuwa /ɛ/ katika lugha ya Kisomali.

Kwa mfano;

**Jedwali 13: Ubadala wa /ɔ/ > /ɛ/.**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Matokeo | Matekeo |
| Ndovu | Ndevu |
| Soma | Sema |
| Chota | Cheta |

Kanuni : /ɔ/ ⟶ /ɛ / / K-K

Sheria tulioitaja hapa juu inaonyesha vokali /ɔ/ inabadilika na kuwa /ɛ/ inapotokea katikati mwa konsonanti. Sauti hizi mbili zinapatikana katikati kundi moja kwa hivyo wasemaji hawa walikanganya sauti hizi mbili wanapozitumia.

Kutokana na mchakato wa vokali inayoonyeshwa katika majedwali, ni bayana kwamba Vokali /a/ inachukua maumbo tofauti katika lugha ya Kiswahili ili kudhihirisha athari hii ya kimofofonolojia. Vokali /a/ inawakilishwa na vokali /e/, /i/, /u/ na /o/. Hali hii inadhihirishwa bayana na kwa mukhtasari katika mchoro ufuatao:

**Mchoro 2: Jinsi /a/ inavyosawariwa na kuwa irabu  tofauti**




Vile vile vokali /ɛ/ inachukua maumbo ya /a/ na /i/ katika lugha ya Kiswahili ili kudhihirisha athari hii ya kimofofonolojia.

**Mchoro 3: Jinsi /ɛ/ inavyosawiriwa na kuwa vokali tofauti**



Ni bayana kwamba michakato ya vokali imesheheni katika utafiti huu. Vokali zimesawiri mageuzi mbalimbali ya kimofofonolojia kama yalivyofafanuliwa katika kila mchakato. Mageuzi haya ndiyo yaliyoibua makosa ya kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili ambayo yanafanywa na wasemaji wa lugha ya Kisomali.

Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba, konsonanti nazo zimesawiri mageuzi katika utafiti huu ambayo yameangaziwa kama yafuatayo.

### 4.7 Mageuzi ya Konsonanti

Konsonanti za lugha ya Kiswahili zimepitia mageuzi wakati zinatamkwa na kuandikwa, na msemaji wa lugha ya Kisomali. Mageuzi haya yamedhihirika katika michakato mbalimbali ya kimofofonolojia inayohusisha konsonanti. Michakato hii ni uchopekaji wa konsonanti, udondoshaji wa konsonanti na udhoofikaji wa konsonanti.

#### 4.7.1 Ubadala wa konsonanti

Baadhi ya konsonanti za maneno ya Kiswahili zimepitia mageuzi na kudhihirisha makosa ya kimofofonolojia yanayofanywa na wasemaji wa Kisomali.

##### 4.7.1.1 Ubadala wa /ʃ/> /č/

Mchakato huu umesawiriwa na maneno yaliyo hapo chini ambayo wasemaji Wasomali wanayatumia yakiwa na makosa ya kimofofonolojia, wanatumia /č/ pale alipokusudia kutumia /ʃ/.

**Jedwali 14: Ubadala wa /ʃ/ > /č/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Shati | Chati |
| Shamba | Chamba |
| Shabiki | Chabiki |
| Shauri | Chauri |
| Shaka | Chaka |

Kanuni : /ʃ/ → /č/ / -i

Kanuni tulioandika inaafiki kuwa /ʃ/ inabadilika na kuwa /č/ inapotoa kabla ya irabu. /ʃ/ inaimarika na kuwa /č/ ambayo inatamkwa kwa sauti kuu. Hii ni kwa sababu sauti hizi mbili hutamkiwa katika kaa kaa gumu. Lakini /ʃ/ ni kikwamizwa na /č/ ni kipasuo-kwamizwa.

**4.7.1.2 Ubadala wa konsonanti /b/ > /p/**

/p/ ilitumiwa pale ambapo /b/ ilipaswa kutumiwa. Mchakato huu ulidhihirisha makosa haya, kama ilivyoonyeshwa katika mifano ifuatayo;

**Jedwali 15: Ubadala wa konsonanti /b/ > /p/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Bangi | Pangi |
| Baadaye | Paadaye |
| Barafu | Parafu |
| Bunduki | Punduki |
| Bao | Pao |
| Bafuni | Pafuni |

Kanuni : /b/ ⟶ /p/ / + i

Kanuni tuliotaja hapo juu inaafiki kuwa /b/ inabadilika na kuwa /p/ inapotokea mwanzoni mwa neno na inafuatwa na irabu. Sauti hizi mbili ni vipasuo na hutamkiwa midomoni kwa hivyo wasemaji hawa wanaonekana kutatizwa na sauti hizi mbili.

**4.7.1.3 Ubadala wa /p/ > /b/**

Konsonanti /b/ ilitumiwa pale ambapo /p/ ilipaswa kutumiwa. Mfanyiko huu wa ubadala ulidhihirisha haya;

**Jedwali 16: Ubadala wa /p/ > /b/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Napenda | Nabenda |
| Nilipoona | Niliboona |
| Akapanua | Akabanua |
| Isipokuwa | Isibokuwa |
| Tulipumzika | Tulibumzika |
| Tulipanda | Tulibanda |
| Amepata | Amebata |
| Upande | Ubande |
| Tupeleke | Tubeleke |
| Popote | Pobote |
| Apate | Abate |
| Hakupata | Hakubata |
| Alipika | Alibika |

Kanuni : /p/ ⟶ /b// i-i

Katika kanuni tulioandika hapa juu inaafiki kuwa /p/ inabadilika na kuwa /b/ inapotokea katikati mwa irabu mbili. Konsonanti hizi mbili ziko katika kundi la vipashuo ambazo hutamkiwa katika mdomo. Konsonanti /p/ ni si ghuna ilhali konsonanti /b/ ni ghuna basi hali inaleta utofauti katika sauti hizi mbili, kwa hivyo wasemaji hawa wanaonekana kukanganya sauti hizi katika matumizi.

**4.7.1.4 Ubadala wa /č/ > /ʃ/**

Konsonanti /ʃ/ ilitumiwa pale ambapo msemaji alitaka kutumia /č/.

Mifano ifuatayo ilidhihirisha haya;

**Jedwali 17: Ubadala wa /č/ > /ʃ/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Mchezo | Mshezo |
| Mchumba | Mshumba |
| Mchele | Mshele |
| Mchoro | Mshoro |

Kanuni : /č/ ⟶ /ʃ/ / K-I

Sheria hii inadhihirisha kuwa /čh/ inabadilika na kuwa /ʃ/ ikitokea katikati mwa konsonanti na irabu. Haya yanadhihirika katika kanuni iliyopo hapa juu.

**4.7.1.5 Ubadala wa /ð/ > /Ɵ/.**

Jedwali 18 linaonyesha kuwa wasemaji wa lugha ya Kisomali wanaotumia lugha ya Kiswahili, watumia / Ɵ / pale ambapo wanakusudia kutumia / ð /. Lugha ya Kiswahili ina fonimu hizi mbili /ð/ na /Ɵ/ lakini lugha ya Kisomali ina fonimu /ð /. Wasemaji hawa walitumia /ð/ badala ya /Ɵ/ kwa sababu hawajui ni wapi inatumika na ni wapi haitumiki katika lugha ya pili.

**Jedwali 18: Ubadala wa : /ð/ > /Ɵ/.**

| Neno sahili | Neno lenye athari |
|---|---|
| Mawaidha | Mawaitha |
| Nidhamu | Nithamu |
| Adhuhuri | Athuhuri |

Kanuni : /ð/ ⟶ /Ɵ/ / i-i

Sheria hii inadhihirisha kuwa /ð/ inabadilika na kuwa /Ɵ/ inapotokea katikati mwa irabu mbili.

Haya yanaafiki kanuni iliyo hapo juu.

**4.7.1.6 Ubadala wa /s/ > /z/.**

Konsonanti /z/ ilitumiwa pale ambapo msemaji alikuwa amekusudia konsonanti /s/.

Mfano ufuatao unadhihirisha mfanyiko huu.

**Jedwali 19: Ubadala wa /s/ > /z/.**

| Neno sahihi | Neno lenye athari |
|---|---|
| Siafu | Ziafu |
| Sanduku | Zanduku |
| Sifa | Zifa |
| Siku | Ziku |

Kanuni : /s/ ⟶ /z/ / -I

Kanuni tuliotaja hapo juu inaafiki kuwa /s/ inapotokea mwanzoni mwa neno kabla ya irabu hubadilika na kuwa /z/. Haya yanaafiki kauli iliyo hapa juu.

#### 4.7.1.7 Ubadala wa /z/ > /s/.

Msemaji alitumia /s/ pale ambapo alikuwa anataka kutumia /z/ hili lilitatiza kupata maana ile ilikuwa imekusudiwa.

Mifano iliyopo hapa chini inadhihirisha haya.

**Jedwali 20: Ubadala wa /z/ > /s/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Zamani | Samani |
| Zote | Sote |
| Zenu | Senu |
| Zao | Sao |
| Zangu | Sangu |
| Zaka | Saka |
| Zetu | Setu |

Kanuni : /z/ ⟶ /s/ / -I

Sheria tuliotaja inaafiki kuwa /z/ inabadilika /s/ inapotokea mwanzoni mwa neno na inafuatwa na irabu. Wasemaji Wasomali wanatumia /s/ kwa sababu katika lugha ya Kisomali sauti /z/ hakuna kwa hivyo wajipata wakitumia iliyokaribiana na hiyo.

#### 4.7.1.9 Ubadala wa /ɲ/ > /j/

Wasemaji wa lugha ya Kisomali walitumia /j/ pale ambapo walitaka kutumia /ɲ/. Hali hii ilitatiza kuelewa kwa maana.

Mifano ifuatayo ilidhihirisha mfanyiko huu.

**Jedwali 21: Ubadala wa /ɲ/ > /j/**

| Neno sahihi | Neno lenye athari |
|---|---|
| Nyumba | Yumba |
| Nyani | Yani |
| Nyasi | Yasi |
| Nyuma | Yuma |
| Nyingi | Yengi |
| Nyufa | Yufa |

Kanuni : /ɲ/ ⟶ /j/ / -I

Kanuni hii inadhihirisha kuwa /ɲ/ inabadilika na kuwa /j/ inapotokea mwazoni mwa neno na inafuata irabu. Kauli iliyo hapa juu inaafiki haya.

**4.7.1.10 Ubadala wa /ʃ/ > /s/**

/s/ ilitumika pale ambapo msemaji wa Kisomali alikuwa anataka kutumia /ʃ/.

Mifano ya kudhihirisha hili.

**Jedwali 22: Ubadala wa /ʃ/ > /s/**

| Neno sahihi | Neno lenye athari |
|---|---|
| Shangazi | Sangazi |
| Shauri | Sauri |
| Shamba | Samba |
| Sherehe | Serehe |
| Shirika | Sirika |
| Shule | Sule |

Kanuni : /ʃ/ ⟶ /s/ / -i

Katika sheria hii ni dhahiri kwamba /ʃ/ inabadilika na kuwa /s/ pale ambapo inatokea mwanzoni mwa neno na inafuata irabu.

**4.7.1.11 Ubadala wa /f/ > /b/**

/b/ ilitumiwa pale ambapo /f/ ilipaswa kutumika katika maogezi. Jedwali hili hapa chini linaafiki haya.

**Jedwali 23: Ubadala wa /f/ > /b/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Fora | Bora |
| Faulu | Baulu |
| Fanya | Banya |
| Finya | Binya |

Kanuni : /f/ ⟶ /b/ / -i

Kanuni tuliotaja inaonyesha kuwa /f/ inabadilika na kuwa /b/ pale ambapo inatokea mwanzoni mwa neno na inafuata irabu.

**4.7.1.12 Ubadala wa /v/ > /f/**

/f/ ilitumiwa katika mazungumzo wakati msemaji alikuwa anataka kutumia /v/. Mifano ya maneno. Jedwali lililo hapa chini linaafiki haya.

**Jedwali 24: Ubadala wa /v/ > /f/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Vizuri | Fizuri |
| Vita | Fita |
| Vuta | Futa |
| Viatu | Fiatu |
| Vifo | Fifo |

Kanuni : /v/ ⟶ /f/ / -I

Kanuni tuliotaja inaafiki kuwa /v/ inabadilika na kuwa /f/ pale ambapo inatokea mwanzoni mwa neno na inafuata irabu. Hili linatokea kwa sababu wasemaji Wasomali hawana /v/ kwa hivyo wanahamisha kanuni za lugha yao katika lugha ya Kiswahili.

#### 4.7.1.13 Ubadala wa /g/ > /k/

Konsonanti /k/ ilitumiwa katika mazingira ya /g/ katika mazungumzo ya wasemaji wa Kisomali. Mifano hii ilidhihirisha mfanyiko huu.

**Jedwali 25: Ubadala wa /g/ > /k/.**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Zangu | Zanku |
| Yangu | Yanku |

Kanuni : /g/ ⟶ /k/ / K-I

Kanuni hii inadhihirisha kuwa konsonanti /g/ inabadililika na kuwa /k/ inapotokea katikati mwa konsonanti na irabu.

#### 4.7.2.1 Uchopekaji wa konsonanti

Katika mchakato huu tulibainisha makosa ya kimofofonolojia, konsonanti zilichopekwa katika maneno ya lugha ya Kiswahili, mwanzo na kati mwa neno. Konsonanti mbalimbali za lugha ya Kiswahili zimechopekwa kama ifuatavyo:

**4.7.2.2Uchopekaji wa /j/**

Konsonanti /j/ imechopekwa katika maneno mbalimbali kama ilivyobainika kwa mifano ifuatayo.

**Jedwali 26: Uchopekaji wa /j/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Ongea | Ongeya |
| Ikaingililia | Ikaingililiya |
| Kufurahia | Kufurahiya |
| Alifurahia | Alifurahiya |
| Familia | Familiya |
| Anasomea | Anasomeya |
| Sijaiona | Sijaiyona |

Kanuni : /ø/ ⟶ /j/ / i-i

Sheria tuliotaja inadhihirisha kuwa /j/ inachopekwa katikati ya irabu mbili ambazo zinafuatana.

**4.7.2.3 Uchopekaji wa /w/**

Konsonanti /w/ ilichopekwa katika maneno na kuleta athari ya Kisomali. Mifano ifuatayo inadhihirisha mchakato huu.

**Jedwali 27: Uchopekaji wa /w/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Tulitoa | Tulitowa |
| Nililia | Nililiwa |

Kanuni : /ø/ ⟶ /w/ / i-i

Kanuni tulionyesha hapa juu inadhihirisha kuwa /w/ inachopekwa katikati pale ambapo irabu mbili zinafuatana.

#### 4.7.2.4 Uchopekaji wa /n/

Konsonanti /n/ ilichopekwa katika maneno ya Kiswahili wakati msemaji wa Kisomali alikuwa akitumia lugha ya Kiswahili. Mifano ifuatayo ilidhihirisha mchakato huu;

**Jedwali 28: Uchopekaji wa /n/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye makosa** |
|---|---|
| Rudi | Rundi |
| Kidogo | Kidongo |
| Mafuta | Mafunta |

Kanuni : /ø/ ⟶ /n/ / I-K

Kanuni tulionyesha hapa juu inadhihirisha /n/ inachopekwa katikati ya irabu na konsonanti wakati wasemaji Wakisomali wanapotumia lugha ya Kiswahili.

#### 4.7.2.5 Uchopekaji wa /h/

Konsonanti /h/ ilichopekwa katika maneno ya Kiswahili wakati msemaji wa Kisomali alikuwa akitumia lugha ya Kiswahili. Mifano ifuatayo inadhihirisha hili:

**Jedwali 29: Uchopekaji wa /h/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Elimu | Helimu |
| Arifa | Harifa |

Kanuni : /ø/ ⟶ /h/ / -I

Katika kanuni iliyoonyeshwa hapa juu /h/ inachopekwa mwanzoni mwa neno ambalo linaanza kwa irabu.

**4.7.3.1 Udhoofikaji kwa konsonanti**

Konsonanti pia zimedhoofika katika kuonyesha athari za kimofofonolojia. Kwa jinsi ambavyo zimeonyesha kupungua katika nguvu za kuzitamka konsonanti zilizodhoofika ni zifuatazo.

**4.7.3.2Kudhoofika kwa konsonanti /j/ hadi irabu /i/**

Konsonanti /j/ inayopatikana katika lugha ya Kiswahili imegeuzwa wakati wa kutamka na kuandika kama /i/ wakati wasemaji Wasomali anatumia lugha ya Kiswahili. Maneno yaliyohusika na mageuzi haya yamedhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 30: Kudhoofika kwa konsonanti /j/ hadi irabu /i/**

| **Neno sahihi** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Vyombo | Viombo |
| Kulevya | Kulevia |

Kanuni : /j/ ⟶ / i/ / K-I

Kanuni hii inaonyesha /j/ inadhoofika na kuwa /i/ inapotokea katikati ya konsonanti na irabu.

#### 4.7.3.3 Kudhoofika kwa /w/ hadi irabu /u/

Konsonanti /w/ inayopatikana katika lugha ya Kiswahili imegeuzwa na kuwa /u/ wakati wasemaji wa Kisomali anatumia lugha ya Kiswahili. Maneno yaliyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 31: Kudhoofika kwa /w/ hadi irabu /u/**

| **Neno sahili** | **Neno lenye athari** |
|---|---|
| Kwanza | Kuanza |
| Kwenda | Kuenda |
| Kwea | Kuea |
| Swala | Suala |

Kanuni : /w/ ⟶ /u/ / K-I

Sharia hii inadhihirisha kuwa /w/ inadhoofika na kuwa /u/ pale ambapo inatokea katikati ya konsonanti na irabu.

### 4.8 Maelezo ya Matokeo ya Data

Tumeorodhesha fonimu za lugha ya Kiswahili na lugha ya Kisomali, tumegundua kuwa fonimu za konsonanti za lugha ya Kiswahili ni ishirini na tano (Massamba, 2004) na fonimu za konsonanti za lugha ya Kisomali ni ishirini na moja (Koffi, 2012).

Hii ni kumaanisha lugha ya Kiswahili imezidi lugha ya Kisomali kwa fonimu sita ambazo ni /p/, /z/, /ɲ/, /tʃ/, /ɵ/ na /v/ vile vile lugha ya Kisomali ina fonimu tatu ambazo lugha Kiswahili haina: /G/, /ħ/ na /ʕ/. Basi kwa kuzingatia mfumo wa fonimu za konsonanti lugha hizi mbili zinafanana kwa kiwango cha asilimia 43.18 %. Fonimu za irabu katika lugha zote ni sawa, tano kama zilivyojadiliwa awali.

Makosa ya kimofofonolojia yameibuka katika kazi zote za Kiswahili za watafitiwa wetu. Makosa haya yalihusu utumiaji wa ubadilishanaji wa fonimu, uchopekaji wa fonimu na

udondoshaji wa fonimu, jambo ambalo lilipelekea kupotoka au kupotezwa kwa maana lengwa ya wanafunzi wa L2. Tutaeleza sababu za matokeo hayo.

### 4.8.1 Ubadilishaji

Hii ni mbinu ambapo sauti ambayo haipatikani katika mfumo wa lugha fulani inabadilishwa na sauti nyingine au sauti inayokaribiana nayo. Ubadilishaji wa fonimu ni mfanyiko uliovumbuliwa katika kazi za wanafunzi wakati wa utafiti huu. Mchakato huu ndiyo ulichangia makosa mengi kwa mujibu wa utafiti huu. Mfano ni ubadilishaji wa /s/ na sauti /z/, /f/ na /v/ kwa mfano badala ya kuandika [zamani] wanaandika kama [samani], katika kuandika [vaa] wanajipata wakiandika [faa]. Hii ni kwa sababu wasemaji wa lugha ya Kisomali hawana sauti /z/ na /v/ na wanajaribu kutumia sauti inayokaribiana. Hali hii hivyo basi huishia kupotosha maana iliyokusudiwa kwa sababu katika mifano iliyo jadiliwa awali mwanafunzi badala ya kusema zamani kumaanisha kale, neno alilolitumia ni samani linaloeleza vifaa vinavyotengenezwa kwa mbao.

Hali hii imetokea katika maneno mengi ya ya lugha ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya Kisomali. Matumizi ya fonimu mbadala katika ujifunzaji wa lugha ya pili miongoni mwa mwanafunzi wengi ni tatizo sugu. Wanafunzi wasemaji Kisomali hutatizwa na utamkaji au uandikaji wa lugha ya Kiswahili hutegemea muundo wa kiisimu wa L1.

Uchanganuzi wetu wa makosa ya kimofofonolojia yaliyoibuka kwenye kazi za Kiswahili za watafitiwa wetu unaonyesha wazi kuwa wanafunzi wasemaji Kisomali wametumia fonimu za irabu mbadala. Makosa haya yamebainika wazi wazi kwenye data ya kimaandishi kuliko kwenye mazungumzo.

Watafitiwa hawa walipendelea kutumia /Ɛ/, /i/, /u/ na /ɔ/ mahala pa /a/ , hii ni sababu fonimu /a/ huhitaji nguvu nyingi kutamka. Pili walipendelea kutumia irabu hizo nne zaidi kuliko fonimu /a/ hii ni usahilishaji lugha.

Watafitiwa pia walitumia fonimu konsonanti mahala /ʃ/ pa /č/, /Ө/ mahala pa /ð/, /s/ mahala pa /z/, /ɲ/ mahala pa /j/, /s/ mahala pa /ʃ/ , /f/ mahala pa /v/, /b/ mahala pa /p/ na /k/ mahala pa /g/. Wanafunzi wazungumzaji wa Kisomali walitumia /ʃ/ mahala pa /č/ walipokuwa wakitumia lugha ya Kiswahili. Fonimu /č/ haipatikani katika lugha ya Kisomali basi walitumia iliyokaribiana na ambayo ni /ʃ/ . Matumizi ya fonimu hii yalipelekea kupotoka kwa maana iliyokusudiwa, huu ndio uhawilishaji wa lugha ya kwanza.

Wanafunzi wazungumzaji Kisomali walitumia fonimu /s/ mahala pa /z/, tukumbuke kwamba lugha ya Kisomali haina fonimu /z/. Hivyo basi, ukosefu wa fonimu hii katika lugha ya kwanza ya wanafunzi hawa ni kizuizi haswa cha utamkaji faafu katika lugha ya Kiswahili. Badala ya fonimu hii wanafunzi huishia kutumia fonimu ambayo inapatikana katika L1 yao mahala pa fonimu ya L2. Kukanganywa huku kunaletwa na uhawilishaji lugha, tatizo la kuhamisha mfumo wa L1 ya wanafunzi hadi L2 ni sugu miongoni mwa wanafunzi wengi. Tunaweza kusema kwamba wengi wa wanafunzi wa L1 hushnidwa kabisa kumudu matamshi ya L2 hata baada ya ujifunzaji wa miaka mingi. Fonimu /s/ ilitumiwa mahala pa /ʃ/, wanafunzi hawa walitumia kwa sababu walitaka tu kufanikisha mawasiliano.

Uchanganuzi wetu ulibainisha wazi kuwa wanafunzi wasemaji wa Kisomali walitazwa na matumizi ya fonimu /ð/ mahala pa /Ө/. Lugha ya Kisomali haina fonimu /Ө/, lakini lugha ya Kiswahili ina fonimu hizi mbili.

Ukosefu wa fonimu hii katika lugha ya Kisomali ulileta kizuizi cha kimaandishi sawa katika lugha ya Kiswahili. Badala ya hii wanafunzi waliishia kutumia fonimu inayopatikana katika L1. Utata huu unaletwa na uhawilishaji lugha.

Uchanganuzi wa makosa ya watafitiwa wetu umedhihirisha kuwa matumizi ya fonimu /f/ badala ya /v/ yameibuka katika data yetu. Lugha ya Kisomali haina fonimu /v/ lakini lugha ya Kiswahili ina fonimu hizi mbili. Ukosefu huu wa fonimu fulani katika mfumo wa isimu wa L1 ya wanafunzi ndio haswa chimbuko la utata. Utumiaji wa fonimu /f/ ni uhawilishaji wa L1,

kwenda kwa lugha ya Kiswahili hili lilidhihirika zaidi katika kimaandishi kuliko kimazungumzo. Kulingana na jedwali la 4.7.1.2 na 4.7.1.3 watafitiwa wengi wametumia fonimu /b/ mahala pa fonimu /p/ na fonimu /p/ mahala pa /b/. Fonimu /p/ haipatikani katika lugha ya Kisomali lakini fonimu /b/ hupatikana, kutokana na ukosefu huu watafitiwa wanatumia kipasuo lipuzi /b/ ambacho kinapatikana.

Corder (1981) anaeleza kuwa utendaji makosa katika ujifunzaji wa L2 uangaliwe kwa makini kwa sababu unamwezesha mwanafuzi wa L2 kufikia umilisi wa L2. Corder anaonyesha kuwa mwanafunzi anayejifunza L2 ana kosa la umilisi na kosa la utendaji.

Sauti hizi mbili zinawakanganya sana wanafunzi wasemaji lugha ya Kisomali wanapojifunza Kiswahili kama L2, kwani mwanafunzi anajipata ametumia fonimu tofauti. Hali hii husababishwa na uyabisi:

Kwanza ni usukukaji wa kiisimu hasa pale mwanafunzi anatumia /b/ kama /p/. Selinker (1972) anasema kuwa wanafunzi wa L2 punde yu wanakumbana na mifumo geni wao huwasilisha mfumo wa L1 hadi L2. Pili, usahilishaji lugha kupitia uundaji lugha kati ya wanafunzi hawa. Iribemwangi (2008) anaelezea kuwa lugha kati ni ile wanayotumia wanafunzi wa L2 kabla ya umilisi kamilifu wa L2.

Aidha kuna baadhi ya wanafunzi hawa ambao hupendelea kutumia fonimu /k/ mahala pa /g/, fonimu hizi mbili zinapatikana katika lugha ya Kisomali na Kiswahili. Wanafunzi hawa walifanya hivo kwa kuwa fonimu /k/ katika lugha ya Kisomali ni kipasuo tulivu, basi hakihitaji nguvu nyingi kutamkwa tukilinganisha na fonimu /g/ ambayo ni kipasuo lipuzi kwa hivyo kinahitaji nguvu nyingi kutamka. Tunaweza kudai kuwa walifanya hivyo kama mkakati wao wa kufanikisha mawasiliano kupitia lugha ya Kiswahili ambayo ni L2 yao.

Baadhi ya watafitiwa walitumia fonimu ya irabu /i/ badala ya fonimu ya konsonanti /j/ na fonimu irabu /u/ badala ya fonimu konsonanti /w/. Utata huu wa kiisimu mara nyingi ulidhihirika kiothografia, wanafunzi hawa hufanya hivi ili kuhifadhi muundo ndani wa

maneno katika othografia ya Kiswahili. Aghalabu uhifadhi huu wa muundo ndani wa maneno ni mgumu kusikika katika utamkaji wa lugha kadirifu. Mfanyiko huu unaibua utata pale ambapo, kwa mfano, wanafunzi wa Kiswahili wanapokumbana na maneno kama vile [vyombo] wanaandika [viombo], [kwea] wanaandika [kuea] na kadhalika.

## 4.8. Udondoshaji

Massamba (2009) anaeleza udondoshaji kama utaratibu wa kutoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi. Kwa hivyo tunaweza kusema udondoshaji ni kanuni inayohusu kuachwa kwa sauti fulani katika matamshi wakati mofimu mbili zinapokaribiana yaani katika mazingira hayo ya sauti ambayo ilikuwepo hapo awali hutoweka. Kwa mujibu wa maelezo haya utafiti huu ulichunguza udondoshaji wa fonimu katika maneno ya Kiswahili unaotokana na athari ya Kisomali. Uchanguzi uliofanywa unathibitisha kuwa wanafunzi wengi wanaotumia Kisomali wanadondoa sauti kama vile /i/, /ɛ/, /ɔ/, /h/ na kadhalika, sababu kuu ya udondoshaji huu ni kuwa lugha ya Kisomali ni lugha bainishi ambayo maneno yake huwa na silabi funge mifano ya maneno ni kama *qalin, sarir, miss, tinn* na mengine mengi. Basi zikitokea katika lugha ya Kiswahili huwa zinadondoshwa na wanafunzi wengi ili kuchukua mfumo wa Kisomali na kusababisha athari katika lugha ya Kiswahili.

Udondoshaji wa irabu miongoni mwa wanafunzi wazungumzaji wa Kisomali ulilenga kuunda silabi funge kimaandishi na kiutamkaji.

Hali hii ilipunguza idadi ya silabi katika maandishi ya L2, kutokana na uchanganuzi wa data ni wazi kuwa watafitiwa walidondosha fonimu zifuatazo irabu /i/, /a/, /ɛ/ na /u/. Udondoshaji huu wa fonimu za irabu katika maneno ya Kiswahili uliibua miundo ya silabi funge katika uandikaji na utamkaji. Isitoshe miundo ya silabi kama hii husheheni kwenye L1 ya wanafunzi hawa. Hali kama hii huletwa na michakato kama vile usukukaji wa kiisimu na upinishaji.

Miundo ya silabi ni kama vile ***KKI***, umedhihirika katika lugha kadirifu kwa mfano ***m-ta-nga-zo*** badala ya ***ma-ta-nga-zo*** na ***mas-ki-o*** badala ya ***ma-si-ki-o***. Iribemwangi (2010) anasema

kwamba lugha bainishi hukumbwa na miundo ya silabi funge kama vile IK na KIK. Hivyo Kiswahili kinapokopa misamiati kutoka lugha bainishi huibuka na miundo kama hiyo ya silabi

### 4.9 Uchopekaji

Massamba (2009) anasema uchopekaji ni uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno. Hivyo basi kwa maelezo sahihi tunaweza kusema kuwa uchopekaji ni hali ambapo kitamkwa kinaingizwa mahala popote katika mfululizo wa vitamkwa vingine ambavyo vipo tayari katika neno. Mfanyiko huu unasaidia lugha kuoanisha matamshi ya maneno na mfumo wa kifonolojia, hasa, kwa kuzingatia misingi ya silabi za lugha husika. Aghalabu vitamkwa vinavyochopekwa vinaweza kuwa na manufaa ama visiwe na manufaa hasa pale ambapo misingi ya mfanyiko huu huwa una asili katika lugha ya kwanza. Utafiti huu unathibitisha uchopekaji ambao unatokana na athari ya lugha ya kwanza ya Kisomali na hivyo kuwa na athari katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Uchanganuzi wa data tulionyesha kuwa wanafunzi wasomali wanaojifunza lugha ya Kiswahili huchopeka kiyeyusho katika maneno ya Kiswahili. Lugha za Kiswahili na Kisomali zina sauti /w/ na /j/ hivyo si ngeni kwa wanafunzi hawa wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Uchopekaji wa sauti hizi umebainika kuwa mwingi miongoni mwa wanafunzi hawa. Lugha ya Kisomali inapendelea muundo funge wa silabi na hauruhusu mfuatano wa sauti za irabu. Wanafunzi wasomali hujaribu sana kuepuka mfuatano wa sauti za irabu katika Kiswahili kama ilivyo katika lugha ya Kisomali. Wao hufanya hivi kwa kuchopeka kiyeyusho kati ya irabu mbili. Aghalabu uchopekaji huu wa viyeyusho hulenga kuivunja mifuatano ya irabu katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wanafanya ili kuhawilisha muundo wa silabi unaopendelewa na L1 hadi L2.

Uchanganuzi wa data ulionyesha kuwa watafitiwa wengi walitatizwa sana na matumizi ya fonimu /h/ wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Japo sauti hii inapatikana katika lugha ya Kisomali lakini iliwatatiza mno katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hali ilisababishwa na mifanyiko ya kifonolojia inayohusu irabu za lugha ya Kisomali. Wanafunzi hawa hujaribu

kuhawilisha muundo wa konsonanti na irabu ndefu, yaani: {KI:}. Muundo huu husheheni katika maneno mengi ya lugha ya Kisomali. Wanafunzi hawa hufanya hivi kwa kutumia mikakati miwili ya ujifunzaji lugha ya pili. Michakato hii ni usukukaji wa LI ya watafitiwa na usahilishaji lugha. Uhawilishaji wa lugha ya Kisomali hadi lugha ya lugha ya Kiswahili unahusu muundo wa silabi.

Data ambazo tumezichanganua zimeonyesha kuwa fonimu /n/ ilichopekwa visivyo katika kazi za watafitiwa walipokuwa wakijifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Athari hii ilionekana wazi hususan katika data za kimaandishi. Fonimu hii katika lugha ya Kisomali hutumiwa kama sauti mwambatano na fonimu /t/, /g/, /d/. Hivyo wasemaji wa Somali wanafanya fonimu /t/, /g/ na /d/ kuwa nazali kwa kuongeza sauti ya nazali /n/ ili kuwiana na mtindo wa lugha ya Kisomali. Hali hii ililetwa na ufundishaji mbaya wa othografia ya lugha ya Kiswahili.

## 4.11 Kihitimisho

Kutokana na utafiti huu inadhihirika kuwa kuna athari ya Kisomali katika lugha ya Kiswahili. Chanzo cha athari ni utofauti katika mifumo ya lugha hizi mbili, iligunduliwa ya kuwa Kiswahili sanifu ina konsonanti ishirini na tano ilhali lugha ya Kisomali ina konsonanti ishirini na mbili kwa mujibu wa (Koffi, 2012). Konsonanti /G/, /ħ/ na /ʕ/ zinapatikana katika lugha ya Kisomali na hazipo katika lugha ya Kiswahili.

Konsonanti /p/, /Ɵ/, /č/, /ɲ/, /z/ na /v/ zinapatikana katika lugha ya Kiswahili na hazipo katika lugha ya Kisomali. Kwanza tunapata udondoshaji wa sauti ambapo nyingi za sauti zinazodondoshwa kwa kuwa maneno mengi huwa yanaishia kwa konsonanti. Kwa hivyo wasemaji wa lugha ya Kisomali wanajipata wakidondosha maneno ya lugha ya Kiswahili wanapoizungumza. Baadhi ya mifano inayodhihirisha hili ni: kijan, asubuh, baday, kakang, na maneno mengine kama yalivyoelezwa awali. Hii ni kwa sababu lugha ya Kisomali ni silabi funge.

Mfanyiko wa pili uliojitokeza kutokana na utafiti huu ni ule wa uchopekaji. Aidha sauti ambazo hazipatikani katika Kisomali zinazalishwa na kuleta athari katika lugha ya Kiswahili. Uchopekaji huu huwa hauna manufaa yoyote kwa sababu asili yake ni katika lugha ya kwanza na hivyo huchangia katika makosa mengi. Mifano ya maneno yanayotokana na mfanyiko huu ni kama rundi, mafunta, niliamkwa, ongeya, furahiya na maneno mengine kama yalivyodhihirishwa awali.

Mfanyiko wa tatu ni ubadilishaji wa fonimu katika kazi za wanafunzi wakati wa utafiti huu. Mchakato huu ndiyo ulichangia makosa mengi kwa mujibu wa utafiti huu. Mfano ni ubadilishaji wa /s/ na sauti /z/, /f/ na /v/ kwa mfano badala ya kuandika zamani wanaandika kama samani, katika kuandika vaa wanajipata wakiandika faa.

Hii ni kwa sababu wasemaji wa lugha ya Kisomali hawana sauti /z/ na /v/ kwa hivyo hawajui tofauti na huenda wakazichanganya. Hali hii hivyo basi huishia kupotosha maana iliyokusudiwa kwa sababu katika mifano iliyo hapo juu mwanafunzi badala ya kusema zamani kumaanisha kale, neno alilolitumia ni samani linaloeleza vifaa vinavyotengenezwa kwa mbao. Utafiti huu unaonyesha pia baadhi ya wanafunzi walifanya makosa kwa sababu hawakujua kanuni za lugha ya Kiswahili. Tatizo hili linadhihirika kutokana na namna wanafunzi hao walivyounda sentensi zao katika insha.

Hatimaye ni muhimu kutaja kuwa utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi makosa ni nadharia ambayo hutumiwa kusaidia kutambua makosa na kurekebisha. Katika muktadha huu makosa yaliyotambuliwa ni ya lugha ya Kiswahili yanayosababisha na athari ya lugha ya Kisomali wakati wasemaji wa lugha ya Kisomali wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Maelezo ya kina yalitolewa awali kuhusu sauti za lugha hizi mbili jambo ambalo limesaidia kutambua athari. Matokeo yalisaidia kuonyesha sauti zilizosababisha athari katika lugha ya Kiswahili kutoka kwa lugha ya Kisomali. Utafiti pia unaonyesha kuwa unaweza kubashiri sauti za Kisomali ambazo zinaweza kusababisha athari katika Kiswahili.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Kitangulizi

Katika sura hii tumefafanua jinsi maswali yetu ya utafiti yalivyojibiwa na data tuliyopata kutoka nyanjani, kupitia kwa kujadilili michakakato ya kiisimu. Kila mchakato tumeutolea mifano mingi. Pia utafiti huu unapaswa kutia mori watafiti wa baadaye.

## 5.2 Hitimisho

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti mawili. Kwanza kabisa, utafiti huu umetekelezwa ili kuweka wazi kwamba kuna athari za kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili zinazotokana na lugha ya Kisomali. Makosa yaliyopatikana katika uchanganuzi huu yalitokana na insha ambazo wanafunzi waliandika. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, imedhihirika kwamba lugha ya Kiswahili ina makosa ya kimofofonolojia yanayosababishwa na umilisi wa lugha ya Kisomali. Makosa haya yalipatikana kwa wingi. Baadhi ya makosa haya ni kama [asubuh badala ya asubuhi], [samani badala ya zamani], [ serehebadala ya sherehe] na mengine mengi.

Tumejadili michakato mitatu mikuu ambayo ilijitokeza katika matumizi ya maneno mbalimbali katika uandishi wa insha na usimuliaji wa hadithi. Michakato iliyoshughulikiwa ni: udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu. Hii ni hali ambayo hujitokeza kutokana na haja ya watafiti wahusika kutaka kurahisisha ujifunzaji wa lugha ngeni kwa kutumia misingi ya lugha yao ya kwanza. Matokeo ya matumizi husika ya lugha ni kuvyazwa kwa maneno ambayo hayakubaliki katika Kiswahili Sanifu.

Utafiti huu ulibainisha kuwa makosa ya kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili kutoka lugha ya Kisomali yanahusu michakato inayopitiwa na maneno haya.

Michakato hii ni ya kimofofonolojia ambayo inahusisha fonolojia na mofolojia ya maneno kutoka lugha hizi. Kwa hivyo maumbo ya maneno ya Kiswahili hayabadiliki yenyewe bali huongozwa na kanuni za kimofofonolojia inayofanyika katika maneno ya Kiswahili ili kudhihirisha makosa hayo. Mifanyiko ya kimofofonolojia iliyodhihirika katika athari hii ni

uchopekaji wa konsonanti na irabu, ubadilishaji wa vokali na konsonanti na udondoshaji wa konsonanti na vokali.

Uchopekaji wa sauti fulani katika maneno ya Kiswahili, unaweza kuelezwa kuwa na asili yake katika lugha ya kwanza. Hii ni kwa sababu sauti fulani inachopekwa pale ambapo haipatikani katika mfumo wa lugha ya kwanza kwa hivyo inabidi msemaji wa lugha ya kwanza kutumia sauti inayokaribiana na hiyo katika lugha yake.

Utafiti huu pia ulivumbua kuwa sauti katika lugha ya Kiswahili zinadondoshwa na wasemaji Wasomali na kusababisha athari katika lugha ya Kiswahili. Hili linatokea kwa kuwa baadhi ya maneno ya Kisomali hushia na konsonanti. Ubadilishaji wa fonimu unatokea pale ambapo fonimu katika lugha ya Kisomali haipo au inakaribiana na nyingine pale msemaji anapotumia lugha ya Kisomali.

**5.3 Mapendekezo**

Utafiti huu hauwezi kudai kwamba umeshughulikia athari za Kisomali katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kikamilifu bali ni matumaini yetu kwamba tafiti zingine zitaweza kutalii masuala haya na mengine kama vile athari zinazotokana na tofauti za kisarufi baina ya lugha hizi mbili. Baadhi ya makosa yaliyojitokeza yalikuwa ni ya ngeli. Mfano ni katika insha moja ambapo mwanafunzi aliandika, *gombe yalikula*, badala ya *ng'ombe alikula*.

Hii inatokana na tafsiri ya moja kwa moja ya lugha ya Kisomali. Hivyo basi tafiti katika sintaksia zitakuwa na manufaa kwa wanaisimu zikifanywa.

Ni muhimu kutambua kuwa katiba ya Kenya inazitambua lugha zetu za kiasili. Hivyo basi tafiti kuhusu lugha zetu za kwanza zinapaswa kuendelezwa kwa marefu na mapana. Utafiti huu umechunguza chanzo cha athari ya makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa Wasomali. Data iliyo katika utafiti huu, hivyo basi itakuwa na manufaa makubwa kwa walimu pamoja na wanafunzi kwa sababu watakuwa na marejeleo ya kuwaauni kuepuka makosa ya tahajia yanayotokana na lugha ya kwanza. Aidha kupitia data hii walimu wataweza kuwaelekeza wanafunzi na kuwafundisha tofauti za mifumo ya lugha hizi mbili.

Inapendekezwa kuwa walimu waelewe nadharia wanazotumia katika ufunzaji wao. Kwa kufanya hivi wanafunzi watapewa mazoezi katika maneno ambayo wanaweza kubashiri yataleta athari hasa kupitia nadharia ya uchanganuzi makosa. Utafiti huu ulijikita katika mofofonolojia na itakuwa bora ikiwa uchunguzi mwingine utafanywa ili kutafiti ngeli za nomino.

**MAREJELEO**

Adam, J. na Kamuzoro, F. (2007) *Research methods for Business and Social Studies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Anderson , B. (1972) *Contributions to Generative Phonology*. Austine London: University of Texas Press.

BAKIZA. (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Bartoo ,J. P.(2004) Acquisition of English Syntax by Keiyo L1Speakers .Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), ChuoKikuu cha Egerton, Kenya.

Bosha,I. (1993) *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya.* Dar esSalaam: Dares Salaam University Press.

Chimerah, R. (2002) *Kiswahili Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: University of Nairobi Press.

Chiragdin, S. na Mnyampala, M. (1997) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: O.U.P.

Cohen , L. na Morrison , K. (2000) *Research Methods in Education* . Toleo la 8. London: Rutledge Falmers.

Conway, E. (2013) An Analysis of Somali Pronunciation Errors. (Unpublished) M.A Thesis Hamlire University, Minnesota.

Corder, S. (1974) *Error Analysis: Perspective on Second Language Acquistion.* London: Longman.

Cross, S. (2009) *Diagnosing the Process, Text and Intrusion Problems Responsible for L2 Listeners' Decoding Errors. In the Asian EFL Journal Quarterly. Vol. 2 Issue (Uk. 47-50)* Asian EFL Journal Press, Busan, Korea. http://www.asian-efl-journal.com.

Dulay,H. na Burt,M.(1974) You can't Learn without Goofing. InJ.C.Richards (Mh.), *Error Analysis*. London:Longman.

Ellis, R. (1985) *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.

Els, T. et al. (1994) *Applied Linguistics and the Learning and Teaching of Foreign Languages.* London: Edward Anorld.

Fromkin,V.,Rodman,R.,naHyams,N.(2007)*AnIntroductiontoLanguage(8th ed.).* Boston,MA:ThomsonWadsworth.

Guthrie, M. (1948) *The Classification of the Bantu languages*. London: OUP.

Hagège,C.(1999)TheChildbetweenTwoLanguages.InM.Karra,(2006) *SecondLanguageAcquisition:Learners'ErrorsandErrorCorrectioninLanguageTeaching*.RetrievedMay22, 2007fromhttp://www.proz.com/doc/633.

Habwe, J. na Karanja, P. (2009) *Misingi ya Kiswahili*.Nairobi:Phoneix Publishers.

Iribemwangi , P. (2010)*The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag

Iribemwangi , P. na Mukhwana , A. (2001) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.

James, C. (1980) *Contrastive Analysis*. Longman, Burnt Mill Harlow.

John, O. (2009) *Elements of Education & Social Science Research Methods*, Maseno, Kenezja Publisher.

Lakkis, K. na Malak, M.(2000) UnderstandingtheTransfer of Prepositions*Forum, Vol38, No3*. Retrieved inMay22nd,2007 fromhttp://exchanges.state.gov/ forum/vols/vol38/no3/p26.htm

Kasomo, D. (2010) *Research Methods in Humanities and Education : Qualitative and Quantitative Research made simple*. Nairobi :Lap Lambert Academic Publishing.

Kevogo, A., Kitonga, N., and Adika, S. (2015) Multingualism and Language Use Patterns: on Humanities and Social Sciences Volume 5, No. 4, 2015

Kihore, Y., Massamba, D. na Matangila , M. (2001)*Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam TUKI.

King'ei, K. (2010) *Misingi ya Isimujamii*. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Kothari, K. (2009) *Research Methodology* . New Delhi: New Age International (P) Limited

Lado, R. (1957) *Linguistics Across Cultures.*Michigan: The University of Michigan Press.

Lamberti, M. (1986) *Die Somali-Dialekte*. Hamburg: Helmet Buske Publishing

Mangwa, D. (2005) *AtharizaKikisiikatikaKiswahilinaZinavyochangiaMatokeo MabayayaMtihaniwaKitaifawaKiswahilikwaWanafunziWakisiiWilayani KisiiKusini*.Tasnifuya M.A(Isiyochapishwa),ChuoKikuu cha Egerton,Kenya.

Massamba, D. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Massamba, D., K ihore, Y. na Hokororo, J. (2009) *Sarufi Miundo ya Kiswahili.* Dar es Salaam:TUKI.

Mbaabu, I. (1995) *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*.Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.

Mgullu, R. (2001) *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mochiwa,Z.(1979).TheImpactofKiswahiliLanguageonEthnicLanguages:A CaseStudyfromHandeniDistrict.TasnifuyaM.A.(Isiyochapishwa),Chuo Kikuu cha Dares Salaam,Tanzania.

Mohamed, A. (2013) An Overview of the Interface between Aspects of Somali Phonology and Morphology: A Resource Guide for ESL Teachers. (Unpublished) M.A Thesis, St. Cloud University, Minnesota.

Mudhune, S. (1994) Contrastive Analysis to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners. Unpublished M. A Thesis, Kenyatta University,Nairobi.

Mudhune, D. (2008) Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Tigania, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Egerton University.

Munyua, J. (2002) The Emerging Viswahili and Kiswahili Research Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur.97–107). Eldoret: Moi University Press.

Ndungu ,I. (1999) *Kikuyu Learners of English as Second Language*: Tasnifu ya Uzamifu: Nairobi: UON.

Ngugi, J. (2007) Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu : Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru. Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya

Nunan, D. (1992)*Research Methodology in Language Learning*. Cambridge: Cambridge University Press.

Olive,M. na Abel, G. (2011) *Research Methods: Quantitative and Qualitative approaches*. Nairobi: Acts Press

Onyango, J. (1997)Uziada wa Kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi Linganuzi.Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta , Nairobi.

Pia, J. (1965) Somali Sound and Inflections. (Unpublished PhD), Indiana University, Bloomington , United States of America.

Prasad, T. (2012) *Acouse in Linguistics*. New Delhi: PHI Learning Private Limited.

Rapondo , M.(2005)Makosa ya Kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi, Tansifu ya Uzamali (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Saeed, J. (1999) *The Focus Structure of Somali*. Philadephia :John Benjamins Publishing.

Schane, S. (1973*) language Change and Generative Phonology*. Oxford: Oxford University Press.

Selinker, L. (1972)*Inter Language*. New York: Rawlence erlibaum associates, INC (RAL).

Sture, J. (2010) *Ethics in Research Project*. Some Guidance on Recognising and Addressing Ethical Issues. Bradford: University of Brandford Press.

Taylor, B. (1975) The Use of Overgeneralization and Transfer Learning Strategies by Elementary andI ntermediate Students of ESL. *LanguageLearning, 25:73- 107* .Retrieved in June 7th,2008 from abisamra03. tripod. com/nada/languagea cq-erroranalysis.html.

Van Els, T. et al (1984) *Applied Linguistics and the Learning and Teaching of Foreign Languages.* . London: Edward Arnold.

Willis Y.na David O. (2011). *A General Guide to Writing Research Proposal and Report.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Yule, G. (1985) *The Study of Language*. London: Cambridge University Press.